# Nipashe

Ijumaa Agosti 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580304

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710





Haijawezekana kuzikwa pamoja, wachongewe sanamu maalum

BUFE

IJUMAA AGOSTI 7, 2020 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Ofisa SUA: Biashara ya sungura inalipa nyama, kinyesi, mkojo

Ujangili unaofilisi tembo hifadhini na pigo la 'Operesheni Tokomeza'

Na Sabato Kasika

• Miaka mitano waliuawa asilimia 60
• Leo wapya 80%; watuhumiwa 1,600

Askari wanyamapori wakiwa katika nyendo zao ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. PICHA: MTANDAO

## Jela maisha kwa kulawiti mtoto wa mwaka mmoja

UKURASA 3

UKURASA 11

# JPM ataja sababu kuomba tena urais

UKURASA 2




Mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais John Magufuli na Mgombea Mwenza wake, Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, wakionyesha mkoba wenye fomu za uteuzi wa wagombea wa kiti cha Rais na Makamu wa Rais, baada ya kukabidhiwa na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Semistocles Kaijage (hayupo pichani), jijini Dodoma, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## NDUGAI APIGIWA DEBE U- SPIKA

UKURASA 3

# Waziri kikaangoni tuhuma rushwa kura za maoni CCM

**WAMO** pia DC mstaafu, Mwenyekiti UWT na Katibu aliyedaiwa kutoa fedha ... *Endelea ukurasa wa 2*




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** YANGA YAFUMUA NA KUSUKA UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Waziri kikaangoni tuhuma za rushwa

**Na Thobias Mwanakatwe**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Mary Mwanjelwa, amehojiwa na Kamati ya Usalama na Maadili ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kwa tuhuma za kutoa rushwa wakati wa kura za maoni.

Mbali na Mwanjelwa, wengine waliohojiwa ni aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Chunya mstaafu, Maryprisca Mahundi ambaye aligombea ubunge wa Viti Maalum (CCM) mkoani humo.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, aliliambia gazeti hili jana kuwa mbali na Mahundi, Mwanjelwa ambao walikuwa wakichuana katika kinyang'anyiro hicho, kamati hiyo pia iliwahoji Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake (UWT) Wilaya Mbarali, Zabibu Baharam na Katibu wa UWT Wilaya hiyo, Veronica Mwembezi.

Mwakasole alisema chama kimechukua hatua hiyo baada ya kuwapo kwa tuhuma za wanachama hao kujihusisha na vitendo vya rushwa ambavyo viliopigwa marufuku katika mchakato mzima.

Alisema hatua hiyo imechukuliwa kwa sababu kanuni, maelekezo na maonyo yalitolewa kwamba mgombea yeyote haruhusiwi kutoa rushwa au kupokea mahali popote pale, kufanya hivyo ni kukosa maadili.

"Ni sahihii kuna sauti zilirushwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba baadhi ya watia nia waliwapa rushwa wajumbe wakati wa kura za maoni. Nilichokifanya ni kuitisha kikao cha Kamati ya Usalama na Maadili na tumewahoji wahusika wote," alisema.

"Tuliowahoji kwenye kikao cha Kamati ya Maadili ni Mwanjelwa (Naibu Waziri), Maryprisca Mahundi, Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Mbarali na Katibu wa UWT Wilaya ya Mbarali," alisema.

Mwakasole aliongeza kuwa baada ya kuwahoji, wamepeleka suala hilo kwenye vikao vya ngazi za juu katika chama mkoa ikiwamo Kamati ya Siasa ya Mkoa na kutoa mapendekezo na baadaye litafikishwa kwenye vikao vya juu zaidi kwa uamuzi.

Awali Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Palangyo, alipoulizwa suala hilo alikataa kulitolea maelezo kwa njia ya simu na kumtaka mwandishi kufika ofisini kwake.

Mwanzoni mwa wiki hii, kulisambaa sauti mitandaoni inayodaiwa kuwa ni ya Mwanjelwa akidaiwa kutoa rushwa kwa wajumbe wa Mkutano wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Mbeya ikiwa ni njia ya kushawishi kupata nafasi ya kuingia kwenye ubunge wa viti maalum kupitia CCM.

Ujumbe huyo alikuwa akielezea fedha alizotoa kwa wajumbe zilivyoliwa na viongozi kutoka moja ya wilaya za mkoa huo.

Kwenye ujumbe huo, Mwanjelwa anasikika akimkaripia Katibu wa UWT Wilaya ya Mbarali aliyefahamika kwa jina la Vero, ambaye anadaiwa alipewa Sh. 100,000 kwa ajili ya kumpa kila mjumbe lakini yeye akapunguza na kutoa Sh. 50,000.

Hata hivyo, Mwanjelwa alisikika akisema mpaka kufikia jioni kuamkia siku ya uchaguzi, hakuwa na nia ya kutoa fedha, lakini aliambiwa na wapambe wake kuwa asipotoa mambo yanaweza kuwa magumu kwake kwa sababu wenzake wanatoa.

Mtu aliyefahamika kwa jina la Zabibu, anayedaiwa kuwa Mwenyekiti wa UWT Wilaya, akimweleza Mwanjelwa kwamba katibu hakuwapa wajumbe mzigo alioutoa na badala yake amewapa watu aliowataka tu.

"Wajumbe kibao hajawapa na mimi nimempigia sasa hivi nimemwambia mbona wale watu hujawapa akaniambia hela zilikuja chache nikamwambia hapana," alisema Mwenyekiti huyo huku Mwanjelwa akisikika kwamba fedha zilipelekwa kwenye bahasha zikiwa zimehesabiwa maalum kwa wajumbe, hivyo hakuna uwezekano wa kupotea.

"Naijua Mbarali iko kwenye vidole vyangu. Wajumbe wenyewe nawajua kama navyojua mboni ya jicho langu, najua wako wangapi, kama ni mjumbe wa mkutano mkuu wa taifa, mjumbe wa mkutano mkuu wa wilaya, makatibu nawajua na najua kata ziko ngapi," alisikika Mwanjelwa akizungumza na mtu huyo na kuongeza kuwa:


"Kwanza haitakiwi ijulikane kwamba kuna hela ilikuja kutoka kwangu. Mimi nampigia atoe hela maana italeta maneno, watu wamemwaga mahela sana, watu wanajua na fedha niliyotoa ni halali na nilifanya hivyo baada ya kuona watu wametoa hela, yaani watu wamemwaga mahela mpaka basi.

Mwanjelwa pia alisikika akisema kutoa hela hizo ilikuwa haki yake na hana kawaida ya kubagua watu kwa kuwa hata wale waliokuwa wanamchukia kwenye uchaguzi huo alitaka wote wapate mgawo bila kubaguliwa.

Baada ya mazungumzo hayo, Mwanjelwa alimpigia Vero na kumhoji kwa nini hakutoa mgawo kama ulivyokuwa umepangwa kwa wajumbe.

Aidha, saa chache baada ya kuvuja kwa sauti hiyo, pia kulisambaa mitandaoni sauti inayodaiwa kuwa ni ya Maryprisca Mahundi.

Wakati wa mchakato wa kura za maoni ubunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Mwanjelwa alishika nafasi ya kwanza kwa kupata kura 374, huku nafasi ya pili ikishikiliwa na Mahundi aliyepata kura 336.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, akionyesha kitabu kinachoelezea maisha ya Rais John Magufuli, baada ya kukizindua katika viwanja vya Nyerere Squre jijini Dodoma, jana. Kushoto ni mwandishi wa kitabu hicho, Mathias Kabadi. **PICHA: PAUL MABEJA**

# JPM achukua fomu, aeleza sababu za kugombea tena

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amechukua fomu kugombea tena urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), huku akiweka bayana sababu za kuomba ridhaa ya kuongoza nchi kwa mara ya pili.

Akizungumza jana katika makao makuu ya CCM jijini hapa baada ya kuchukua fomu katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema moja ya sababu za kufanya hivyo ni kumalizia viporo vilivyobaki na kuifanya Tanzania kuwa kama Ulaya.

Magufuli alieleza mambo mengi ambayo yamefanyika kwa kipindi cha miaka mitano ya uongozi wake na Watanzania watarajie maajabu zaidi iwapo watampa ridhaa ya kuongoza tena kwa kipindi kingine cha miaka mitano.

"Kitabu cha Ilani ya Uchaguzi safari hii ni kikubwa sana kushinda miaka mitano iliyopita, maana yake kina mambo mengi sana. Siwezi kuyasema yote tutayasema siku ya uzinduzi wa kampeni na nawaomba viongozi wenzangu uzinduzi wa kampeni uanzie Dodoma kwa kuwa ndiyo makao makuu ya nchi," alisema.

Kila eneo nchini, alisema kuna kitu cha maendeleo kimefanyika huku akitolea mfano ujenzi wa shule za msingi 908 na za sekondari 228 ambazo zimejengwa kwa kipindi cha miaka mitano.

"Tulipochaguliwa kuongoza taifa hili, yako mengi tumefanya ni mengi sana. Yanahitaji siku, mwezi, mwaka kuyaelezea kila mahali. Kila utakapogusa, vituo vya afya karibu 500, stendi ni nyingi mno zilizojengwa na zinaendelea kujengwa," alisema.

Rais Magufuli alibainisha kuwa ameomba nafasi hiyo si kwa kulazimishwa bali anatambua ana wajibu wa kuwa mtumishi wa wanyonge na wanaoteseka vijijini huku akisema mtu hawezi kuzungumza maendeleo ya viwanda bila kuwa na umeme.

"Unapozungumzia viwanda umezungumzia ajira kwa kuwa vijana wengi wa kitanzania hawana ajira kutokana na hakuna viwanda vya kwenda kufanya kazi. Lakini ili viwepo viwanda vinahitaji umeme, ndiyo maana nikasema liwalo na liwe lazima tujenge mradi mkubwa wa Stieglers Gorge ambao utatoa megawati 2115. Tukiwasha huu umeme bei itapungua," alisema.

"Tumechoka taifa hili unasafirisha pamba kama malighafi inakwenda nje na wakitengeneza nguo wanaleta zilizovaliwa. Sisi tunataka tukilima pamba yetu tutengeneze hapa hapa kwenye viwanda vyetu kwa kutumia umeme wetu na zile nguo tunawapelekea na ikiwezekana tuwapelekee ambazo zimevaliwa," aliongeza.

Pia alisema mazao ya kilimo na mifugo yote yatachakatwa nchini ili kutengeneza ajira kwa vijana.

"Haya nimeyaona ndiyo maana nikasema nichukue miaka mingine mitano niyaendeleze haya, nikilitumikia taifa kama mtumishi wenu. Tumechezewa sana kwenye madini. Wapo watu ambao walizungumza hadharani kwamba tutashughulikiwa na tutanyooshwa. Nilisimama na wana CCM nikasema ni bora kufa, lakini unaifia nchi yako kwa sababu tumechezewa sana," alisema.

Awali, Rais Magufuli alifika saa 4:00 katika ofisi za NEC kuchukua fomu akiwa ameambatana na mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan, na viongozi wengine wa chama wakiwamo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Akitoa maelezo ya awali kabla ya kukabidhiwa fomu hizo, Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema tume imeandaa fomu namba 8A ambayo inatumika kwa ajili ya uteuzi wa wagombea kiti cha Rais na Makamu wa Rais.

Alitaja baadhi ya sifa zitakazotumika kuamua kumteua mgombea kuwa ni pamoja na kutotiwa hatiani na mahakama yeyote kwa kosa lolote la kukwepa kulipa kodi ya serikali.

Akimkabidhi fomu hiyo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji (mstaafu) Semistocles Kaijage, alisema katika mkoba wa fomu kuna nakala nane za fomu namba 10 ya tamko la kuheshimu na kutekeleza maadili ya uchaguzi.

HABARI KITAIFA

# Ndugai apigiwa debe u-Spika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amempigia debe Spika wa Bunge, Job Ndugai, akisema atashangaa kama Bunge lijalo hawatamchagua kushika wadhifa huo kutokana na mambo makubwa aliyofanya ikiwamo kutungwa kwa sheria bora ya madini.

Magufuli alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Makao Makuu ya chama hicho, baada ya kuchukua fomu ya kuomba kugombea urais katika Tume ya Taifa ya Uchaguzi(NEC) kupitia CCM.

"Namshukuru sana Spika, nitashangaa sana bunge linalokuja wakaacha kukuchagua wewe. Watasema nakupigia kampeni, nina haki kwani uliunda Tume ya Madini kwenda kuchunguza na ripoti akaileta na tukabadilisha sheria," alisema.

Sheria hiyo, alisema ni sheria bora nchini kwa kuwa madini sasa yanapatikana na fedha zinazotokana na rasilimali hiyo zinapelekwa kwenye miradi ya maendeleo.

"Tunaijenga nchi yetu ndiyo maana leo mnaona hata Mmasai Laizer anapata madini ya kilo 10. Zamani mbona yalikuwa hayaonekani? Hii ni kwa sababu tumejenga ukuta ndiyo maana ndugu zangu wana CCM katika kufikiria haya kwamba tumehangaika hivi, tukiondoka wale wenye rangi nyingine ambayo si ya kijani watakuja kuyafanya haya.

"Walikuwa wanashirikiana na mabeberu kutuibia madini yetu leo kweli wataweza kulinda madini yetu? Ndiyo maana nimesema potelea mbali nagombea miaka mingine mitano. Tanzania hii ni taifa tajiri, lakini tulizoeshwa kuambiwa maskini ndiyo maana tumeingia kwenye uchumi wa kati na tumeingia kwa sababu mali yetu ilikuwa inaibwa sasa tumeidhibiti vizuri.

Naye Spika Ndugai alimhakikishia Rais Magufuli kuwa atapata kura nyingi Dodoma na nchi nzima kutokana na mambo aliyoyafanya.

Makamu wa Rais na Mgombea Mwenza, Samia Suluhu Hassan, alisema vifo vya wanawake na watoto vilivyokuwa vinaliliwa vimepungua kwa kiwango kikubwa.

"Tulikuwa tunalia na vifo vya wanawake vimepungua kwa kiasi kikubwa, tatizo la maji kwa asilimia 74 limepungua. Tulikuwa tunalia tatizo la ada kwa watoto wetu umetupokea huo mzigo tunashukuru sana, umetung'arisha katika majumba yetu mapya hadi vijijini kwenye matembe kwa kutuletea umeme," alisema.

Awali, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ali, alisema mitambo ya ushindi kwa chama hicho imewashwa rasmi jana huku akitaja majukumu ya jumuiya za chama hicho katika kuhakikisha ushindi wa kishindo unapatikana.

"Kuhamasisha wananchi kupiga kura nyumba kwa nyumba, kitanda kwa kitanda, mtaa kwa mtaa, shuka kwa shuka na kulinda kura jukumu hili tumelikabidhi kwa Jumuiya ya Vijana wa CCM(UVCCM)," alisema.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akiangalia na kufurahia nyundo na kijembe, wakati alipotembelea banda la maonyesho la Chuo cha Mafunzo Zanzibar, wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya Wakulima Nanenane, katika viwanja vya Chamanangwe, Wilaya ya Micheweni Pemba jana. **PICHA: IKULU**

# Jela maisha kwa kulawiti mtoto wa mwaka mmoja

**Na Samson Chacha,** TARIME

MFANYAKAZI wa nyumbani, Magige Thomas (21), mkazi wa Mtaa wa Rebu, Tarime mjini mkoani Mara, amehukumiwa kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia ya kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi 5.

Hukumu hiyo imetolewa na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya ya Tarime, Veronika Mugendi, aliyesikiliza kesi hiyo ya jinai namba 419 ya mwaka 2019.

Kabla ya kusomwa kwa hukumu hiyo, Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Inspekta Salum, alidai mahakamani kuwa, mtuhumiwa huyo mnamo Agosti 5 mwaka jana mchana, akiwa mfanyakazi wa nyumbani maeneo ya Bomani, wakati wazazi wa mtoto huyo wakiwa wamekwenda kazini, alimlawiti mtoto wa mwajiri wake na kumsababishia maumivu makali. Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulipeleka mashahidi wanne na kuithibitishia mahakama kuhusiana na kitendo hicho ikiwamo taarifa za polisi (PF3), mganga na wazazi na upande wa utetezi haukuwa na shahidi utetezi uliotolewa na mshtakiwa.

Hakimu Mugendi alisema kuwa, kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa mbele ya mahakama yake, anaungana na upande wa mashtaka na kumtia hatiani mtuhumiwa Magige na kumhukumu kwenda kutumikia kifungo cha maisha jela, ili liwe fundisho kwa watu wenye nia ovu na wasio na huruma na watoto.

Licha ya mshtakiwa kuiomba mahakama kumsamehe makosa yake au kumpa adhabu ndogo, Mwendesha Mashtaka wa Polisi Salum aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa mtuhumiwa kwa kuwa kitendo alichokifanya ni cha kinyama.

Baada ya hukumu hiyo kutolewa, mtuhumiwa alionekana akitokwa machozi, huku wananchi waliokuwa wamefurika mahakamani hapo kufuatilia hukumu hiyo, wakisikika wakisema 'haki imetendeka'.

Kumekuwa na ongezeko la matukio ya ukatili dhidi ya watoto nchini, baadhi ya wataalamu wa saikolojia na ustawi wa jamii wakidai hali hiyo inachagizwa na mambo mengi zikiwamo imani za kishirikina na jamii kutokuwa na hofu ya Mungu.

TEF

TANZANIAN ELEPHANT FOUNDATION

P. O BOX 6502, KILIMANJARO, TANZANIA

AGA KHAN ROAD, 3rd FLOOR, KILIMANJARO NSSF COMMERCIAL COMPLEX

215847001

TAARIFA KWA UMMA

Tanzanian Elephant Foundation (TEF), ni shirika lisilo la kiserikali linalojihusisha na uhifadhi wa tembo Tanzania kupitia tafiti za kisayansi, kudumisha mshikamano baina ya watu na tembo pamoja na utoaji wa elimu ya uhifadhi wa tembo na wanyamapori kwa ujumla.

Shirika linapenda kuwatangazia umma wa watanzania na wanufaika wote wa maeneo ya mradi kwamba tumepokea ufadhili kwa ajili ya kutekeleza mradi kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020.

| No: | Mfadhili | Shughuli | Muda wa mradi | Fedha za mradi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | PRINCE BERNHARD NATURE FUND (PBNF) | Kudumisha mshikamano baina ya watu na tembo kupitia miradi ya kuongeza kipato na elimu katika jamii zinazopakana na hifadhi ya taifa ya Nyerere, Tanzania. | 07/2020-06/2021 | Tsh. 46,000,000/= |

Email: info@tef.or.tz, Website: www.tef.or.tz

# VETA yabuni kifaa cha upandaji mbegu

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MBUNIFU wa kifaa cha kupanda mbegu mbalimbali shambani kutoka VETA Kihonda Morogoro, Gema Ngoo, amesema upandaji wa mbegu kwa njia ya kawaida ya mkono kunapoteza mbegu nyingi zaidi wakati wa kupanda.

Mbunifu huyo aliyasema hayo jana wakati wa utoaji elimu ya matumizi ya kifaa cha kupandia mbegu kwa wananchi waliotembelea banda la VETA viwanja wa Nanenane, Nyakabindi mkoani Simiyu.

Alisema ili kuepuka upotevu wa mbegu shambani ni vyema wakulima wakatumia kifaa hicho ili kupunguza upotevu na muda.

"Wakulima wengi wanatumia muda mwingi na mbegu nyingi shambani, lakini kwa kutumia kifaa hiki wataokoa muda na upotevu wa mbegu na itakuwa msaada mkubwa kwao kwa kuwa watavuna kwa tija kulingana na ukubwa wa shamba," alisema.

Alisema kifaa hicho kina uwezo wa kupanda hekari tatu kwa siku kwa kutumia nguvu za binadamu.

Baadhi ya wakulima waliofika katika banda hilo kujionea teknolojia mbalimbali, walisema wamefurahishwa na elimu inayotolewa VETA kwa kuwa ni mwanga katika uzalishaji wa shughuli zao katika kilimo.

Holo Maduhu, mkazi wa Bariadi, alisema ana uhakika kupitia elimu ya matumizi ya vifaa kazi vinavyobuniwa na mamlaka hiyo vitasaidia kuongeza ujuzi na maarifa.

# Kamwelwe aifunda TANROADS

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ameutaka uongozi wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), kutimiza wajibu wao pasipo kusubiri au kusukumwa na maelekezo.

Alitoa kauli hiyo wakati akifungua mkutano wa kumi na nne wa Baraza la Wafanyakazi wa TANROADS nchi nzima na kusisitiza umuhimu wa kila mtu kwa nafasi yake kutimiza wajibu wake wa msingi katika eneo lake la kazi.

"Tunafahamu changamoto mbalimbali zinazowakabili katika kutekeleza majukumu yenu, lakini niwatie moyo na mwendelee kuchapa kazi kwa moyo wa kizalendo na kutanguliza maslahi mapana ya Taifa na kuhakikisha hakuna jambo lolote linaloweza kukwamisha ama kuzuia utekelezaji wa majukumu yenu," alisema Kamwelwe.

Aidha, aliwataka TANROADS kuendelea kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi mikubwa inayoendelea hapa nchini hasa ile iliyosainiwa hivi karibuni ikiwamo ujenzi wa barabara ya mzunguko wa Jiji la Dodoma, Daraja la Kigongo - Busisi mkoani Mwanza, barabara ya Tanga - Pangani pamoja na miradi mingineyo.

Mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye ni Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Patrick Mfugale, alisema kuwa wakala unaendelea na utaratibu wa kuweka alama mpya za barabara kuu na za mikoa zinazohitajika na kuboresha zile zilizopo ambazo hazikidhi vigezo kwa mujibu wa sheria.

# Wakili Mkuu afunguka utawala wa sheria

**Na Hellen Mwango**

WAKILI Mkuu wa Serikali, Gabriel Malata, amesema ofisi yake iko makini kuhakikisha utawala wa sheria unaimarika na kwamba haitasita kupeleka rufani katika mahakama za juu kwa ajili ya kupata nafuu nyingine wanapoona sheria zinakiukwa.

Kadhalika, amesema ofisi yake ina wajibu na jukumu la kusimamia na kuhakikisha sheria zinafuatwa ikiwamo kuzingatia wajibu na haki zake. Rai hiyo aliitoa jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini Dar es Salaam.

"Ofisi yangu ina haki ya kusimamia utawala wa sheria na haitasita kufungua rufani mahakama za juu kwa sababu tuna wajibu wa kusimamia na kuhakikisha sheria husika zinafuatwa," alisema na kuongeza:

"Nasikitika kuona baadhi ya mawakili ambao wanapinga maamuzi ya Mahakama nchini kwamba inashindwa kusimamia katiba, sisi mawakili tunafahamu njia za kufuata pale tunapohitaji nafuu ya mahakama na si kudhihaki na kuitusi kwenye mitandao ya kijamii au vyombo vya habari."

Alisema mawakili wajibu wao ni kuisaidia mahakama na si kuibeza bila kujiingiza katika mivutano ya muhimili huo na endapo hawajaridhishwa na maamuzi wakate rufani au watafute namna ya kuomba nafuu kwa mujibu wa sheria.

Aliongeza kuwa kama jamii inadai sababu za kupelekwa kwa maombi hayo ni ubambikiziwaji wa kesi, lazima uwapo ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai hayo, na kwamba katika kesi hiyo hoja hiyo haijazungumzwa. Aidha, alisema katiba kama sheria mama inapaswa kutafsiriwa kwa mapana yake kwa kuzingatia malengo, maudhui yake katika kulinda haki ya kila mtu na jamii kwa ujumla na kwamba ikitafsiriwa bila kuhusisha sheria nyingine ni rahisi kuleta sintofahamu katika jamii.

Alisisitiza kuwa utaratibu wa kuzuia dhamana ni wa kikatiba kwani wakati ibara ya 15(1) ya katiba inampa mtu haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru, ibara ya 15 (2) inaruhusu haki na uhuru wa mtu kuingiliwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria lengo ni kulinda haki na usalama wa jamii.



Waatamiwa katika kituo cha ubunifu cha PASS – AIC, kilichopo TALIRI Kongwa, mkoani Dodoma, wakijifunza mbinu za kunenepesha mbuzi kituoni hapo, juzi. Asasi hiyo, imekuwa ikitoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana nchini, hasa katika ufugaji na kilimo cha kisasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC Jokate awapa kazi maalumu vijana 150

**Na Romana Mallya,** KISARAWE

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, amewataka vijana 150 wanaopewa mafunzo ya akiba wilayani hapa, kutoa taarifa za kikundi au watu wanaohamasisha kuvuruga amani ya nchi kuelekea Uchaguzi Mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Mwegelo alitoa agizo hilo jana wilayani hapa alipofungua mafunzo hayo ya miezi minne kwa vijana hao ambao miongoni mwao wanawake ni 62 na wanaume ni 88 wenye umri wa kuanzia miaka 18 hadi 25.

Mwegelo alisema lazima vijana wawe walinzi wa nchi yao kwa kuweka uzalendo mbele badala ya kuwa sehemu ya kurubuniwa.

"Kuna watu wanalilia amani tuliyonayo Tanzania, kamwe msiruhusu mtu awapotoshe mkahamasika kufanya vitu vya kipuuzi na kuharibu amani ya nchi," aliagiza.

Mwegelo alisema vyombo vya ulinzi na usalama wilayani hapa watafuatilia yoyote atakayejaribu na watamshughukilia kisawasawa na kuwataka vijana hao wasiwe sehemu ya kurubuniwa.

"Tunaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu, mkisikia mtu anayehamasisha kuvuruga amani ya nchi yetu, toeni taarifa, mkawe masikio na macho ya viongozi huko mtaani, kama kuna kikundi au watu wanataka kufanya kinyume, toeni taarifa kwa viongozi," aliagiza.

"Utii, uaminifu, uzalendo na uhodari, kama hizi sifa hauna, hata usome shahada zote ndani na nje ya nchi, utakuwa hufai katika jamii. Mtii serikali na mkawe raia wema, mkalinde rasilimali za taifa na kuzihifadhi, ninategemea hadhi ya uraia wenu itapanda kwa uaminifu mtakaouonyesha baada ya mafunzo haya."

Mshauri wa Jeshi la Akiba Wilaya ya Kisarawe, Meja Mohamed Wawa, alisema mafunzo hayo wakati yanaanza, yalikuwa na jumla ya vijana 158, lakini watano walikutwa na matatizo ya kiafya na watatu ni watoro.

Alisema vijana hao hawajawekwa kambini, bali wamekuwa wakiendelea na mafunzo wakitokea nyumbani.

Alisema hayo moja ya malengo ya mafunzo hayo ni kuwaandaa vijana kuwa wazalendo kwa nchi yao na kuwa sehemu ya utoaji wa taarifa kwa mambo ambayo yako kinyume cha sheria za nchi.

Alisema kati ya vijana 150 wanaoendelea na mafunzo, 50 hawana vyeti vya kuzaliwa, tatizo ambalo Mkuu wa Wilaya, Mwegelo aliahidi litatatuliwa, akimwagiza Katibu Tawala wa Wilaya kulishughulikia.

## TAWIRI yatoa elimu ulinzi wa shoroba

**Na Renatha Msungu,**
BARIADI

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), imetoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kulinda mapito ya wanyamapori, maarufu shoroba, na kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji nchini.

Cecilia Leweli, mtafiti wa wanyamapori kutoka TAWIRI, katika maonyesho ya Nanenane yanayoendelea mkoani hapa, alisema jana kuwa kumekuwa na uharibifu wa shoroba katika maeneo mbalimbali, jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na ustawi wa wanyamapori.

"Tunatumia maonyesho haya kuhakikisha elimu inawafikia wakulima na wafugaji, tunataka waache kuharibu shoroba ili wanyama wapate sehemu za kupita," alisema Leweli.

Alifafanua zaidi ya kuwa uharibifu wa shoroba unachangia pia mazao kuharibiwa na mifugo kitu ambacho huchangia migogoro mingi baina ya pande hizo mbili ambacho TAWIRI inahitaji kuiondoa kati ya wakulima na wafugaji.

Neema Kilimba, mtafiti mwingine wa TAWIRI, alisema elimu na mbinu mbalimbali za kuishi na wanyamapori zinahitajika ili kusaidia kuepusha binadamu kuumizwa na wanyama.

Alisema kumekuwa na migogoro baina ya wanyamapori na binadamu ambapo kila mmoja anakuwa adui kwa mwenzie, lakini anaamini elimu ya kuishi na wanyama itasaidia kumaliza tatizo hilo.

**WIZARA YA FEDHA**

Wakati wananchi wakipewa elimu kuhusu umuhimu wa shoroba, Wizara ya Fedha na Mipango inayatumia maonyesho hayo kutoa elimu ya matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika malipo ya serikali.

Ofisa TEHAMA wa wizara hiyo, Emmanuel Maendaenda, alisema mfumo huo, maarufu GePG, unasaidia kuongeza uwazi na udhibiti wa mapato na kutoa taarifa sahihi za mapato ya serikali.

Alisema mfumo huo umeunganishwa na taasisi zote za umma zinazotoa huduma kwa umma kwa wananchi pamoja na njia zote za kufanyia malipo kama vile benki, wakala wa malipo na mitandao yote ya simu.

# CUF yamchagua mgombea pekee Tunduru

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

WAJUMBE wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), wamewachagua watia nia wa chama hicho kwenye nafasi za ubunge wilayani hapa na Jimbo la Tunduru wajumbe wamemchagua mwanachama pekee aliyejitokeza.

Akitangaza matokeo hayo Msimamizi wa uchaguzi huo, Katibu wa CUF Mtwara Mjini na Mjumbe wa Sekretarieti ya CUF Taifa, Said Kulega, alisema Jimbo la Tunduru Kusini kulikuwa na mgombea mmoja, Ally Mandunda aliyepata kura 206. Alisema wajumbe wa uchaguzi huo walikuwa 209 na kati ya kura zote zilizopigwa, tatu ziliharibika.

Upande wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, kulikuwa na wagombea watatu waliotia nia ya kuwania nafasi hiyo na Mariamu Mohammed, alipata kura 98.

Kwa mujibu wa msimamizi huyo wagombea wengine ni Maisara Chipote, aliyepata kura 64 na Rashid Swalehe alipata kura 10.

Jumla ya wajumbe 179 walipiga kura na hakuna kura iliyoharibika. Awali, Katibu wa CUF, Mtimbalugono, aliwaeleza wagombea hao kuwa matokeo hayo ni ya awali na kuwataka wajumbe, wanachama na wagombea, kusubiri maamuzi ya vikao vya juu vinavyotarajiwa kuketi kati ya Agosti 8 na 9, mwaka huu kwa ajili ya kufanya mapitio na kufanya uteuzi wa wagombea.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, wakichagua midoli kwa ajili ya kuchezea watoto majumbani, katika eneo la Ilala Boma, jijini humo, jana. **PICHA: REHEMA MBINDA - TUDARCO**


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collector, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa tajwa hapo chini, mahali dhamana ilipo kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini; Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **MICHAEL CHACHA CHEGERE** | Nyumba ya makazi yenye Hati ya mauziano iliyopo Mtaa wa Yangeyange Kata ya Msongola Manispaa ya Ilala. | 28/8/2020 |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2.Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**NMB Bank plc,**
**Ohio street /Ali Hassani mwinyi Road,**
**P.O.BOX 9213**
**Dar es salaam**
**Tel:+255 222322550**
**Email: Harrieth.Mally @nmbbank.co.tz**

115847802



**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collector, Auctioneer, Commission Agent, Broker & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **First National Bank (FNB),** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya Mdaiwa wao, ambayo ni Nyumba kama zilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **GEORGE MASHAURI** | Nyumba ya makazi yenye Hati na.53645, Kiwanja na.401, Ardhi na.403492, Kitalu 'C' Iliyopo eneo la Kiseke Mjini Mwanza Iiyopo kwa jina la **GEORGE MASHAURI** | 22/8/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**Contact: +255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**First National Bank Tanzania Limited (FNB)**
**Ohio street**
**P.O.BOX 72290,**
**DAR ES SALAAM**
**Contact: +255 713963596**
**0758502628**
**Email: info@fnb.co.tz**

115847702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Salamu zetu kwa wazazi na walezi

**TANZANIA** inaweza kujivuna kuwa ni nchi ambayo licha ya kuwapo kwa corona duniani, taifa hili limenusurika na kuendelea na ratiba ya masomo katika shule za msingi, sekondari na vyuo.

Wanafunzi wake wameendelea na shule na hadi sasa hali ni shwari na ni jambo la kumshukuru Mungu.

Kwa hiyo hiki ndicho kipindi cha kutoa msukumo kwa elimu hivyo wazazi, walezi na walimu waongeze ushirikiano chanya kufanikisha mafanikio ya elimu nchini.

Tanzania ni miongoni mwa nchi chache ambazo sasa zinajivunia kuwa kwenye kundi la uchumi wa kati, hivyo Watanzania tunapaswa kushirikiana kwa pamoja kuipa elimu kipaumbele kwani hata nchi zilizoendelea zilitilia mkazo wa kipekee elimu, hali iliyowawezesha kufikia mafanikio na maendeleo makubwa waliyonayo sasa.

Elimu ndiyo ufunguo wa kila kitu. Ndicho chanzo cha kuwa na uwezo wa kiuchumi, kiteknolojia na hata kifedha nchi zilizoendelea kusimamia maendeleo yake na kutoa mikopo na misaada kwa mataifa yenye uchumi unaokuwa kama Tanzania.

Kwa hiyo ni muhimu wazazi na walezi kushirikiana na serikali na kuona kuwa watoto wanasoma kwa hiari si kwa kushinikizwa.

Tunashauri wasome kwa hiari bila shinikizo la dola wala viongozi wengine wa serikali kwa kuwa iwapo tutawashinikiza kusoma wanaweza kukosa hamasa ya kujifunza kwa bidii.

Wazazi wengine wanawalazimisha watoto wao kujifelisha mitihani ya darasa la saba au kidato cha nne ili wasiendelee na elimu ya sekondari au ya juu na hili linawahusu zaidi mabinti.

Tunawasisizi wazazi na walezi wasiwe vikwazo na kuwazuia watoto wasijizatiti na kusoma kwa bidii hasa wakati huu wakijiandaa kwa mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne.

Wapo baadhi ya wazazi wanaokuwa wagumu kuwapatia watoto wao mahitaji ya msingi ya shule kwa lengo la kuwakwamisha na kuwarudisha nyuma.

Iwapo mchezo huo utaachwa kuendelea unaweza kukwamisha wanafunzi na kuwasababishia kuchukia shule.

Ni kawaida kwa walezi kutumia kisingizio cha umaskini kuwanyima watoto wao mahitaji hayo ili kuwapunguzia kasi ya kusoma hasa wanapokaribia kwenye mitihani ambayo imebakiza miezi michache hilo si jambo jema. Ni vyema wazazi kama hao wakafuatiliwa ili kukomesha mienendo hiyo kwa kuwa sehemu kubwa ya gharama za elimu inabebwa na serikali kupitia kodi za wananchi.

Tunasema hayo kwa sababu wapo baadhi ya wazazi hawatoi mahitaji muhimu kwa watoto wao mfano sare, madaftari, mikoba ya shule, viatu, chakula na hata kuwalipia gharama za kukaa bweni.

Yote haya husababisha kushindwa kupata mahitaji, haya yanakosababisha watoto wao kukwama kusoma na kuishia kuanguka kwenye Mtihani wa Taifa Kidato cha Nne.

Wazazi kutofuatilia maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao ni jambo ambalo linakwamisha ufaulu.

Tunawakumbusha kuwa wana mchango mkubwa kufanikisha maendeleo ya kitaaluma ya watoto wao kutokana na nafasi kubwa waliyonayo kwa watoto.

Ndiyo maana wazazi na walezi ambao hawataki watoto wao wasome, hawatoi ushirikiano katika masuala ambayo yanaongoza thamani kitaaluma kwa watoto wao.

Kwa mfano, kushindwa kukagua kile ambacho mwanawe anajifunza shuleni, kutohudhuria vikao vya wazazi vya kujadili maendeleo ya taaluma ya mwanawe, kutompa hamasa mwanawe kusoma kwa bidii.


Tunawakumbusha mtoto anapokosa uangalizi na ufuatiliaji wa karibu kutoka kwao ni rahisi kufeli masomo.

Wazazi na walezi wakumbuke wana sehemu kubwa ya kupambana na kufanikisha kufikia mafanikio ya kitaaluma hasa wakati huu wa kuelekea kwenye mitihani ya la saba na kidato cha nne.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uzoaji taka bado ni tatizo Mwananyamala

Na Adam Fungamwango

**HIVI** sasa duniani ni miaka mingi imeshapita, elimu kuhusu umuhimu na usalama wa mazingira ni jambo muhimu sana.

Ni muhimu kwa maana kwamba, inatujengea mazingira ya usalama kiafya na mengi yanayoambatana nayo.

Ukitaka kulijua hilo kwa kina, angalia hata hapa nyumbani kwetu, wajibu wa jukumu hilo ajenda ya mazingira iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Kimantiki, pia nakubaliana na kwa maana zote za usemi 'mazingira ni uhai.' Katika moja ya mambo ambayo ni kipaumbele cha sekta hiyo ni usafi wa kuhakikisha hakuna adha ya taka katika maeneo tunayoishi. Nani analibishia hilo?

Lakini inaopokuja katika utekelezaji wake, jibu linaanza kuwa gumu kiasi, kwa sisi tunaoishi hasa mijini ambako kuna ugumu wa kupata maeneo sahihi ya kutosha kukusanya na kuharibu kwa kuchoma moto taka na mambo kama hayo.

Uongozi wa serikali zetu za mitaa uliyaona hayo na kuunda mifumo ya kuyakabili, kuwa na namna au nyenzo kama magari au trekta yanayokusanya, kuzoa na kwenda kutupa taka hizo. Hiyo si mji mmoja au mwingine, bali kote duniani iko hivyo.

Mifumo hiyo ya kukusanya ya taka hupitia mamlaka za mitaa, ambazo huku kwetu inakuwahi katika sura ya ama mamlaka za miji, manispaa, jiji au wilaya, inayokusanya na kutenga maeneo maalum ya kutupa taka hizo.

Nirejee katika eneo la Mwananyamala Kisiwani ambakao nina ushuhuda wake. Utaratibu ulioko mahali hapo ni kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni, kwamba kuna magari ya kampuni binfasi zilizopewa kandarasi ya kuzoa taka na zingine mali ya halmashauri hiyo.

Watu wanagharamia, chini ya usimamizi wa viongozi wa serikali ya mitaa hadi ngazi ya chini kwa mabalozi wanaokusanya malipo kutoka kwa kila mkazi, hapo nikimaanisha mwenye nyumba hadi mpangaji katika nyumba wastani wa shilingi 1,000 kwa kila mwezi kutoka kwa kila mmoja.

Hapo kuna siku maalum zilizotengwa magari kupita katika eneo maalum kunakoelekezwa kukusanya taka ambazo wazoaji wenye vyombo vya usafiri hupita kukusanya taka hizo.

Malalamiko yetu katika sura kuu hapa, ni hasa pale watarajiwa wa kukusanya taka wenye jukumu au kandarasi hiyo hawajitokezi kwa wakati uliopangwa, ilhali huduma yao inakuwa imeshalipiwa.

Huwa tukienda kuuliza kwa viongozi wetu tulio nao jirani, tunapata majibu ambayo ni wazi yako mbali na ukweli stahiki.

Zaidi ya hapo, nikirejea hoja ya watu hao kushindwa kuzoa taka kwa wakati, badala ya kuboresha mazingira, inachukua sura ya upande wa pili kwamba inachafua mazingira zaidi.

Mahali kunakoelekezwa uchafu kukusanywa ni penye makazi ya watu ambako, taka zinapovunda inakuwa balaa. Hali inakuwa mbaya zaidi na imekuwa kawaida wakazi hao jirani wanalalamika mno, pasipo kusikiwa dai au lalamiko lao, sasa huku ni kuboresha mazingira kweli?

Hali inakuwa mbaya pale mvua zinaponyesha, taka zinapovunda na kuzaa mabaya kuliko, harufu inatapakaa mno kila mahali.

Tunajua taka hizi huzolewa na kwenda kumwagwa katika dampo ya Pugu Kinyamwezi, kutokana na miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam, panapo nyenzo bora za usafiri wa kuzoa taka, inapafanya pasiwe mbali zaidi.

Hata kama kuna shida ya msongamano wa magari, basi kazi hii inaweza kufanyika usiku kwa tija zaidi, kuondoa kero hii. Inapaswa tufike mahali halmashauri zetu nchini na si Kinondoni pekee, kuweka maendeleo kutoka katika sura ya ufanisi wa vitendo.

# Masoko ya madini yaingiza bil. 5.5/-

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MASOKO ya madini ya vito na dhahabu mkoani Ruvuma yameingiza zaidi ya Sh. bilioni 5.5 tangu kufunguliwa kwake Mei, 2019.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mndeme, alisema jana kuwa katika kipindi hicho, masoko hayo yaliyoko Tunduru na Songea yamewezesha kununuliwa madini yenye uzito wa gramu 390,936.27.

"Mrabaha uliopatikana katika mauzo hayo ni Sh. 332,093,674.35, ada ya ukaguzi iliyopatikana ni Sh. 55,348,945.72 na kodi ya huduma iliyopatikana katika kipindi hicho ni Sh. 16,604,683.72," alisema Mndeme.

Alisema serikali imeendelea kutekeleza shughuli mbalimbali kwa ajili ya kukuza sekta ya madini katika mkoa wa Ruvuma.

Mndeme alisema sekta hiyo katika mkoa wa Ruvuma, imekua kwa kasi katika maeneo ya uwekezaji hasa leseni za uchimbaji, uzalishaji madini, ajira na makusanyo ya maduhuli ya serikali. Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Jumanne Nkana, alizitaja faida za uanzishwaji wa masoko ya madini nchini kuwa ni wachimbaji wa madini kupata bei nzuri ya madini kutokana na uwazi ulioko sokoni.

Faida nyingine, kwa mujibu wa Nkana, ni wachimbaji kutokuwa na haja ya kutorosha madini kitendo ambacho kilikuwa hatari kwa kuwa kilikuwa kinasababisha wachimbaji kupokonywa madini na serikali pamoja na kukabiliwa na kifungo pindi wanapobainika kutenda kosa hilo.

Pia alisema serikali kupitia sekta hiyo imepata takwimu sahihi za mauzo ya madini na urahisi wa kukusanya mapato yaliyokuwa yakipotea kutokana na utoroshaji wa madini.

"Faida nyingine ni kuongezeka kwa tija ya utendaji kazi kwenye ofisi za madini kutokana na watumishi wa ofisi kufanya shughuli nyingine badala ya kupoteza muda mwingi kuwafuatilia wachimbaji wa madini migodini. Pia serikali inapata takwimu sahihi za uzalishaji na mauzo ya madini na kuongezeka kwa mapato ya serikali yatokanayo na uchimbaji na biashara ya madini pamoja na uwapo wa masoko haya," alisema Nkana.

Katika kutatua changamoto wanazokabiliana nazo wachimbaji wadogo mkoani Ruvuma, serikali inajenga kituo cha umahiri kwa ajili ya kada hiyo.

Mndeme alizitaja faida za kituo hicho kuwa ni uwapo wa takwimu za wachimbaji wadogo katika mkoa, upatikanaji wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo na utoaji wa mafunzo na maarifa kwa wachimbaji kupitia wadau mbalimbali.

Faida zingine za kituo hicho, kwa mujibu wa Mndeme, ni uwapo wa mfumo wa kutathmini mashapo ya madini yaliyopo ili kufanya uchimbaji wenye tija, mikopo na mitaji kwa wachimbaji wadogo, uongezaji wa thamani madini na masoko na utatuzi wa migogoro ya uchimbaji madini inayojitokeza.




Meneja Uhusiano Biashara za Kilimo wa Benki ya NMB, Christian Kihwelo (kulia), akitoa maelezo kwa mmoja wa wateja waliotembelea Banda la NMB, kwenye Maonyesho ya wakulima Nanenane, Kanda ya Mashariki, mjini Morogoro, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EPZA yataka wawekezaji kutumia malighafi za kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji na Mauzo Nje ya Nchi (EPZA), imewataka wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kutumia fursa ya uwapo wa malighafi nyingi za kilimo kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao ili kuongeza thamani na kupata bei kubwa katika soko.

Hadi sasa kuna viwanda 170 ambavyo vimeanzishwa chini ya EZPA nchini na zaidi ya asilimia 40 ya viwanda hivyo vimejikita katika kuchakata na kuongeza thamani ya mazao.

Akiongea kwenye Maonyesho ya Nanenane yanayofanyika kitaifa mkoani Simiyu, Meneja wa Uhamasishaji, Uwekezaji wa EPZA, Grace Lemunge, alisema kuongeza uwekezaji katika viwanda vya uchakataji mazao kunaongeza thamani ya mazao na kumhakikishia mkulima soko la uhakika na ongezeko la kipato.

"Mamlaka ya EPZA inatumia maonyesho ya Nanenane ya mwaka huu kuwahimiza wawekezaji kutumia fursa kubwa iliyopo katika kilimo kuanzisha viwanda vya uchakataji mazao, jambo ambalo litapunguza uuzaji wa mazao ghafi nje ya nchi. Pia italiongezea taifa fedha za kigeni na kuongeza ajira zaidi," alisema.

Alisema mwekezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji ya EPZ na SEZ, anafaidika na motisha maalum inayotolewa na mamlaka pamoja na kurudisha upesi mtaji aliowekeza.

Sekta ya kilimo inaajiri zaidi ya asilimia 70 ya watu na huchangia asilimia 30 ya Pato la Taifa, hivyo uwekezaji katika viwanda vya kuchakata mazao unamhakikisha mkulima soko la uhakika na kuongeza uzalishaji.

"Ushiriki wetu katika maonyesho ya Nanenane ni muhimu sana kwa sababu kilimo ndio ambacho hutupatia chakula na zaidi pia chanzo kikuu cha kipato cha familia nyingi," alisema.

Tanzania bado ina ardhi kubwa ambayo inafaa kwa kilimo na ambayo haijalimwa bado hivyo uwapo wa viwanda vya kutosha vya uchakataji ni kichocheo muhimu wa kuwafanya wakulima waongeze uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mamlaka ya EPZA inafanya kazi kwa karibu sana na viwanda vya kuchakata mazao kama vile dengu, mbaazi na choroko yenye soko kubwa India na nchi nyingine za Asia. Mamlaka huwaunganisha wakulima na viwanda hivyo na kupata soko la uhakika.

Awali, mazao haya yalikuwa yanatumika kwa ajili ya chakula pekee, lakini sasa ni chanzo kikubwa cha mapato kwa wakulima.

Hivi karibuni serikali imeanza ujenzi wa kituo kikubwa cha biashara cha Kurasini ili kuibadilisha na kuifanya sekta ya kilimo kuwa ya kibiashara.

Mradi wa ujenzi wa kituo hicho ambacho kinatarajiwa kuwa kikubwa nchini na katika eneo lote la ukanda wa Afrika Mashariki, unatekelezwa na EPZA kwa thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 60.

# Unyonyeshaji bado tatizo kwa wazazi

**Na Mary Geofrey**

WAKATI dunia ikiadhimisha Wiki ya Unyonyeshaji, imeelezwa idadi ya watoto wanaoanzishiwa kunyonyeshwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi katika kipindi kisichozidi saa moja baada ya kuzaliwa ni asilimia 53 nchini.

Wataalamu wa masuala ya lishe wamebainisha kuwa idadi ya watoto wanaonyonyeshwa maziwa ya mama pekee bila kupewa maji, vinywaji na vyakula vingine katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58.

Takwimu hizo zilitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Elimu na Mafunzo ya Lishe wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Sikitu Kihinga, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kuadhimisha Wiki ya Unyonyeshaji wa Maziwa ya Mama Duniani mwaka huu.

Alisema licha ya kuwa asilimia 97 ya watoto wenye umri chini ya miaka mwili wananyonyeshwa maziwa ya mama, bado kuna kikwazo hicho cha kutozingatia kunyonyesha maziwa ya mama peke yake katika kipindi cha miezi sita ya mwanzo.

"Ninaamini kuwa katika kipindi hiki cha Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani, jamii itakumbushwa wajibu wao mkubwa katika kuwezesha wazazi kufanikisha unyonyeshaji ili kuboresha zaidi hali ya lishe ya watoto," alisema Kihinga.

Alisema kaulimbiu ya Wiki ya Unyonyeshaji inasema 'Tuwawezeshe wanawake kunyonyesha watoto kwa afya bora na ulinzi wa mazingira'.

Alisema kaulimbiu hiyo inahimiza na kukumbusha wajibu wa makundi mbalimbali ya wadau wa lishe kusaidia na kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyochangia baadhi ya wanawake kushindwa kunyonyesha watoto wao kikamilifu.

Alitaja faida za unyonyeshaji kwa wakati kuwa ni kuboresha hali ya lishe, ukuaji na maendeleo yao kimwili na kiakili kwa watoto na kupunguza kasi ya magonjwa ya kuambukizwa na kupunguza vifo vya watoto nchini.

Kihinga alisema faida ya wazazi kunyonyesha ni kupunguza uwezekano wa kupata maambukizi ya saratani ya matiti na via vya uzazi na kuepuka kupata ujauzito mwingine katika kipindi cha miezi michache baada ya kujifungua.

# Mwekezaji AMMZA atakiwa kuchochea unywaji kahawa

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

KATIBU Tawala Mkoa wa Kagera, Prof. Faustine Kamuzora, amemtaka mwekezaji wa kiwanda cha kukoboa, kusaga na kusindika kahawa (AMMZA) kufungua mgahawa utakaosaidia wananchi kujenga mazoea ya kutumia kinywaji hicho. Takwimu za unywaji wa kahawa kwa mkoa wa Kagera ni asilimia 5 pekee ikilinganishwa na uzalishaji wa zao hilo kwa mwaka 2019/20 wa tani 70,000. Alitoa ushauri huo baada ya kupokea taarifa ya kiwanda hicho ikieleza yenye changamoto za miundombinu na uhitaji wa soko la kahawa iliyosindikwa ndani na nje ya mkoa kwa kuwa Mkoa wa Kagera umepakana na nchi tano.

Prof. Kamuzora alisema fursa ya kwanza ni kutengeneza soko la ndani na kuweka asilimia 50 ndani na 50 nje, ili kuondoa changamoto za masoko na kusadia wananchi unywaji wa bidhaa hiyo unaohitajika.

"Kwanza kabisa inatakiwa mzalishaji atambue umuhimu wa unywaji kahawa hiyo na kujenga mazoea ya matumizi ili wananchi waweze kuimarisha afya," alisema.

"Mwekezaji wetu hiki unachokifanya hapa uwaze na kufungua mgahawa kule mjini, ili na wananchi waweze kujijengea mazoea ya kunywa kahawa," alisema Prof. Kamuzora.

Mwekezaji wa kiwanda hicho, Amiry Amza, alisema endapo kutakuwa na nguvu kazi ya kutosha, watumiaji wa kahawa wataongezeka.

Aliongeza kuwa kwa sasa kiwanda kina uwezo wa kutumia tani 300,000 kwa mwaka licha ya kuwa na changamoto za nishati ya umeme na mtaji mdogo wa kukamilisha ujenzi wa miundombinu.

"Endapo nitakamilisha ujenzi na umeme kuwa wenye uhakika, mpango wangu ifikapo 2022 nitaweza kutumia tani 33,000 kwa wiki," alieleza Amza. Alisema uzalishaji huo umefanikisha kuajiri vijana 42, ambao hufanya shughuli mbalimbali za kuwanufaisha.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa reli ya treni ya kisasa (SGR), katika eneo la Tazara, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: TUKUSUMA MWANDEMELELA - TUDARCO**

# Waagizwa kutotoa leseni ununuzi mazao

**Na Neema Emmanuel,**
MWANZA

WAKURUNGEZI wa halmashauri wametakiwa kutotoa leseni ya ununuzi wa mazao kwa wafanyabiashara katika msimu ujao ili wajiunge na soko la bidhaa Tanzania (TMX) kumkomboa mkulima na kumnufaisha na kazi yake.

Maagizo hayo yalitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, wakati wa kikao kazi cha wadau kuhusu ununuzi wa mbegu msimu wa 2020/21 mkoani hapa.

Alisema asilimia 70 ya Watanzania ni wakulima, hivyo watu wote walioko kwenye minyororo wa thamani, lazima waungane ili kumfanya mtu huyo wa msingi alete tija na kunufaika na mfumo wa soko huria.

"Nafasi ya mkulima ni ya muhimu sana lazima afaidike yule aliyekaa kwenye jua na mvua. Suala la yeye kutembea kilometa 50 na debe moja la dengu hilo sikubaliani nalo. Pia hamna leseni kutolewa kwenye nafaka tunafuata stakabadhi ghalani. Kwa Mkurugenzi atakayetoa leseni msimu ujao tutakufa naye kwani wakurungezi ndio chanzo cha migogoro. Pia chama cha ushirika kitambue uchumi huu ni wa mashindano," alisema.

Akizungumzia wakulima kucheleweshewa fedha za pamba, alisema wote walipwe haki zao na kufikia Septemba Mosi, mwaka huu, asitokee mkulima anadai, hivyo lazima apate haki yake halali.

"Wakuu wa wilaya zifanyieni kazi AMCOS (vyama vya msingi vya ushirika) ambazo hazijawalipa wakulima, zikamateni. Hatutaki madeni, mkumbuke hiki ni kipindi cha mpito, kuanzia Januari mfumo utakaotembea ni stakabadhi ghalani," alisema Mongella.

Naye Kaimu Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Nyanza (NCU), Martha Ndetto, alisema msimu wa 2020/21 kupitia AMCOS Mkoa wa Mwanza, unatarajia kukusanya kilo 12,749,900 za dengu.

"Serikali ilitoa maelekezo kuhusu ununuzi wa mazao ya choroko, dengu, mbaazi, soya na ufuta kwa mikoa inayolima mazao hayo kuanzia mwaka huu kufanyika kupitia mfumo wa ushirika. Lengo ni kuhakikisha yanazalishwa na kuuzwa kwa tija na ubora unaotakiwa na kumwezesha mkulima kupata soko la uhakika na lenye bei ya ushindani," alisema Ndetto.

## Mbegu za miti asili zaanza kuhifadhiwa

**Na Ashton Balaigwa,** BARIADI

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeanza kuhifadhi mbegu za miti ya asili inayotumika kwa ajili ya dawa na matunda.

Mbegu hiyo imekuwa katika tishio la kuanza kupotea, hivyo kwa kuanza kuizalisha kutawawezesha wakulima kupata mazao yatokanayo na misitu kwa ajili ya faida ya vizazi vijavyo.

Hayo yalielezwa na Mtafiti wa Kilimo Misitu kutoka taasisi hiyo, Tumbi Tabora, Kassim Masibuka, alipokuwa akizungumza na wakulima waliotembelea vipando vya mazao mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu katika maenyesho ya wakulima yanayofanyika kitaifa katika viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Alisema hatua ya kuhifadhi mbegu hizo za miti ya asili inatokana na miti hiyo kukatwa kwa wingi kutokana na umuhimu wake, huku ikitumika kwa ajili ya matumizi ya nishati, kutengeneza thamani za vitu pamoja na kuni, hivyo kuifanya miti ya asili kuanza kutoweka katika maeneo mbalimbali ya misitu.

Alisema waliwahoji wakulima miti wanayoitumia na kuwapa kipaumbele na kuifanyia utafiti jinsi gani ya kuiotesha na kuipanda kwenye shamba kama itaweza kuota na kuchanganya na mazao ya kawaida.

Alisema miti hiyo ambayo inatumika kwa ajili ya dawa ya asili na mingine kwa ajili za matunda ya asili, mbegu zake zimehifadhiwa na kuanza kufanyiwa utafiti wa kina kuona kama inaweza kuoteshwa tena na kupandwa katika maeneo tofauti nchini kwa kuchanganywa na mazao mbalimbali ya chakula.

Alisema pia wameanza kusindika matunda ya asili ambayo yatazalisha juisi na jamu ambavyo vitaweza kumwongezea mkulima kipato kinachotokana na miti ya matunda ya asili.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geoffrey Mkamilo, alisema jukumu kubwa walilonalo ni kuona matokeo ya utafiti pamoja na teknolojia mpya zinazoibuliwa zinatoka kwenye makabati na kwenda kwa wakulima ili waweze kubadilisha kilimo kutoka cha kujikimu na kuwa cha kibiashara.

Dk. Mkamilo alisema TARI kupitia vituo vyake vya utafiti, imepanga kuzalisha mbegu za mazao yanayohitajika kama malighafi kwenye uchumi wa viwanda na kutaka wakulima kuchangamkia fursa hiyo.

HABARI KITAIFA

# RC Dar awabana makandarasi miradi miwili

**Na Beatrice Moses**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, amewabana makandarasi wa miradi miwili wanaosuasua kukamilisha ujenzi, amewaonya akiwaamuru waikamilishe haraka, vinginevyo watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Kunenge alitoa maagizo hayo baada ya kufanya ziara ya kutembelea miradi minne ambapo miwili kati ya hiyo inasuasua, hivyo amewataka makandarasi hao kuhakikisha wanakamilisha kazi yao ipasavyo.

Alitembelea mradi wa jengo la watumishi wa Manispaa ya Ubungo, Machinjio Vingunguti, Soko la Kisutu na Kituo cha Mabasi Mbezi.

Akizungumzia kuhusu mradi wa jengo la soko la Kisutu, alibainisha hajaridhishwa na kasi ya ujenzi huo, ametoa miezi miwili kwa mkandarasi huyo kukamilisha.

Hakuwa tayari kumpa muda wa ziada mkandarasi huyo aliyetaka aongezewe miezi sita ndipo aukamilishe.

Badala yake alimwamuru mkandarasi huyo kuongeza watu wasaidie kuongeza kasi ya kukamilisha mradi huu kwa wakati uliokusudiwa, kwa kuwa awali ulipangwa kukamilika Agosti 24, mwaka huu mpaka sasa umekamilika kwa asilimia 60.

Kunenge ambaye katika ziara hiyo aliambatana na Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, pia alibainisha kukerwa na kasi ndogo ya ujenzi wa jengo la Manispaa ya Ubungo ambalo linajengwa na Wakala wa Majengo (TBA).

Alisema yeye siyo mgeni kwenye mradi huo kwa kuwa amewahi kuutembelea akiwa Katibu Tawala wa Mkoa, hivyo anatambua jinsi ambayo ucheleweshwaji huo wa kukamilishiwa jengo hilo unavyosababisha changamoto ya upatikanaji wa huduma katika manispaa hiyo.

Alisema TBA iliomba kupewa muda wa wiki sita ili waweze kukamilisha mradi huo, wakidai kuwa hatua zilizobaki kwa muda huo zitakuwa zimekamilika.

Alimwagiza Katibu Tawala kuhakikisha anautembelea mradi huo mara kwa mara ili kuona unavyoendelea, huku akisisitiza kuwa naye atafanya ziara ya kushtukiza ili kufuatilia mradi unavyoendelea.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Beatrice Dominic, akizungumza na Nipashe alifafanua kutokamilika kwa wakati ujenzi huo kumesababisha utoaji wa huduma katika manispaa hiyo kuwa mgumu kwa kuwa ofisi zimewekwa maeneo tofauti badala ya kuwa kwenye jengo moja.

"Ofisi ya afya ipo Sinza, Maendeleo ya Ardhi na Elimu wapo kule kwa Mkuu wa Wilaya eneo la Kibamba wakati Utumishi, Sheria na Wakaguzi wa Hesabu nipo nao kwenye jengo la muda," alisema Dominic.




Mfanyabiashara wa Jiji la Mwanza, Grace Meshaki maarufu Mama Kweka (katikati), akitoa ushuhuda mbele ya Mkurugenzi wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kulia), kuhusu namna benki hiyo, ilivyompatia mkopo mpaka sasa anamtaji wa zaidi ya Sh. milioni 250, katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo na kati, iliyofanyika jijini humo, juzi. Kushoto ni Meneja wa Tawi la NBC Mwanza, Rodgers Masolwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TADB yatoa bil. 1.8/- kwa kiwanda cha dawa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Antony Mavunde, ameeleza jinsi Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) ilivyofanikikisha uzalishaji wa kiwanda cha kutengeneza dawa za mifugo cha Farm Access kwa kutoa Sh. bilioni 1.8.

Akizungumza na waandishi wa habari alipotembelea maonyesho ya Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni jijini hapa jana na kufika banda la kiwanda, Waziri Mavunde alipongeza juhudi zinazofanywa benki hiyo hasa kufanikisha maendeleo ya sekta ya viwanda kikiwamo kiwanda cha Farm Access kilichopo mkoani Dodoma.

"Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza TADB na uongozi wake kwa hatua stahiki na madhubuti kuunga mkono azma ya serikali za kujenga uchumi wa viwanda hapa nchini," alisema Waziri Mavunde.

Alisema benki ilitoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda mpaka uzalishaji wake kuhakikisha utengenezaji na upatikanaji wa kutosha wa dawa za mifugo kiwandani hapo pamoja na kutoa ajira kwa vijana wa kitanzania.

Hatua hii ya kufanikisha ujenzi wa viwanda vya kimkakati kama hiki cha Farm Access zitasaidia sana kupunguza changamoto za dawa zinazowakabili wafugaji na wakulima sambamba na kuchochea ukuaji wa soko la ajira, alisema.

Mbali ya kuvutiwa na bidhaa za kiwanda hicho, Waziri Mavunde alimhakikishia Ofisa Mwandamizi wa Maendeleo wa Kiwanda, Dk. Simon Mphuru, kuwa serikali imejipanga kujenga uchumi unaotegemea viwanda ifikapo mwaka 2025, na kuahidi kukitembelea kiwanda hicho siku chache zijazo.

Aidha, Mavunde aliitaka TADB kuendelea kushirikiana na benki washirika kwa wakulima wa zao la zabibu kumiliki viwanda vidogo vidogo vya kuongeza thamani ya zao hilo. Kwa upande wake, Dk. Mphuru alimweleza Waziri Mavunde kuwa kiwanda kitaendelea na uzalishaji na kuiomba TADB kuendelea kuwawezesha na kuwajengea uwezo wakulima wadogo, ili kufanikisha azma ya ujenzi wa uchumi unaotegemea viwanda.

Tunaishukuru TADB kwa mchango wake mkubwa katika kuleta mageuzi na mafanikio katika sekta za kilimo na viwanda," alieleza.

# Wadau wanolewa kuhusu utumiaji bora mitandao

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Paradigm Initiative Afrika limewakutanisha wadau mbalimbali wakiwamo waandishi wa habari, wanasheria, walimu pamoja na makundi mengine ya kijamii kwa ajili ya kupewa mafunzo kuhusiana na matumizi bora ya mitandao ya kijamii.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa siku mbili juzi jijini Dar es Salaam na kuhusisha wadau wengine wa nchi za Afrika ya Kati ikiwamo Nigeria ambapo walishiriki kwa njia ya mtandao.

Washiriki kutoka Nigeria walisema lengo lao la ushiriki ni kutaka kupata uzoefu kutoka kwa Tanzania ambayo imepiga hatua katika sekta hiyo hususani katika matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

Akizungumza kuhusu matumizi hayo ya mitandao, mratibu wa semina hiyo kutoka Tanzania, Peter Mmbando alisema kwamba ni wakati mwafaka wa kubadilishana uzoefu kati ya Tanzania na nchi nyingine ili kupanua uelewa na kukabiliana na kasi ya ukuaji wa sayansi na teknolojia kwa mahitaji ya baadaye.

Pia aliwasihi watumiaji wa mitandao ya kijamii kuzingatia kanuni, taratibu na sheria zake.

# Wakulima wasaidiwa upimaji afya udongo

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imeanza kuwasaidia wakulima nchini kupima afya ya udongo kabla ya kuanza kuwekeza kwenye kilimo ili kujua aina ya mazao wanayotakiwa kupanda kulingana na eneo husika.

Kupitia mpango huo, TARI imeanzisha mfumo wa kidigitali ambao utawezesha maofisa wa ugani popote walipo kujua ubora wa udongo na aina ya mbolea inayopaswa kutumika katika eneo la mkulima na kumshauri kabla ya kuanza uwekezaji katika kilimo anachokusudia kukifanya.

Akizungumza kwenye darasa maalumu la kuwafundisha wakulima kujua afya ya udongo lilopo katika viwanja vya Maonyesho ya Wakulima vya Nyakabindi mkoani Simiyu, Mtafiti wa udongo kutoka TARI Mlingano, Dk. Catherine Senkoro, alisema kuwa utafiti unaonyesha asilimia 41 ya maeneo ya kilimo nchini yana kiwango kidogo cha mboji, hivyo ni muhimu kupimwa kwa afya ya udongo.

Dk. Senkoro ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo TARI Mlingano mkoani Tanga, alisema mfumo huo wa kidigitali utasaidia kuongeza tija kwenye uwekezaji katika kilimo kwa kuwa kutakuwa na uhakika wa upatikanaji wa chakula baada ya kujua afya ya udongo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema serikali imeleta teknolojia ya mfumo wa kidigitali wa kupima afya ya udongo kwa lengo la kuwasaidia wakulima kuzingatia matakwa ya matumizi ya udongo unaofaa kwa kilimo wanachotaka kulima badala ya kujilimia kiholela.

# 70 wapoteza ajira mgodi wa urani

**Na Stevie Chindiye,** NAMTUMBO

KAMPUNI ya uchimbaji wa madini ya urani ya Mantra Tanzania Limited iliyotegemewa kuanzisha mgodi wa uchimbaji wa madini hayo katika Kijiji cha Likuyusekamaganga wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, imepunguza wafanyakazi 70 kutokana na mgodi kutoanza kufanya kazi ya uchimbaji.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Hadija Pallangyo, alipokuwa akizungumza akiwa Shule ya Msingi Mwenge katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namtumbo. Alisema kampuni imepunguza wafanyakazi wake kutoka 84 mwaka 2014 na kufikia 14 mwaka huu.

Alitaja sababu kubwa ya kupunguza wafanyakazi hao ni pamoja na kupunguza matumizi ya kampuni kwa kipindi hiki ambacho mradi wa uchimbaji wa urani katika Mto Mkuju kutoanza kufanya kazi.

Pallangyo alifafanua sababu ya kuchelewesha kwa uchimbaji wa madini hayo ni kuporomoka kwa bei ya madini hayo katika soko la dunia.

Aidha, alisema licha ya mradi wa kuchimba madini katika Mto Mkuju kutoanza rasmi, kampuni ya Mantra Tanzania Limited inaendelea kushiriki kuchangia shughuli za maendeleo katika sekta ya elimu, afya na mazingira.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Peres Kamugisha, alishukuru kampuni hiyo kwa kuendelea kushiriki kuchangia shughuli za maendeleo.

Kamugisha alitaja ujenzi wa maabara katika Shule ya Sekondari Nasuli na Shule ya Sekondari Nangungu kuwa ni jitihada ya kampuni hiyo ambayo ilitoa fedha za kukamilisha ujenzi wa maabara katika shule hizo.

Naye mwalimu wa kitengo cha walemavu katika Shule ya Msingi Ufundi Namtumbo, Bibiana Adamu, aliishukuru Mantra kwa kukitembelea kitengo cha wenye ulemavu kujionea changamoto na kuahidi kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu.



Katibu wa Benki ya Stanbic, Hellen Makanza (kushoto), akiwa na Mwasisi, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Watoto Wetu Tanzania (WWT), Evans Tegete (wa tatu kulia) wakati akikagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa madarasa katika kituo hicho kijiji cha Msata, Chalinze mkoani Pwani hivi karibuni. Jengo hilo linajengwa na Benki ya Stanbic kwa lengo la kuunga mkono jitihada za serikali katika sekta ya elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafanyabiashara wadogo wanufaika mikopo NBC

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MFANYABIASHARA wa jijini Mwanza, Grace Kweka, ambaye amenufaika kupitia Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), amewataka Watanzania kutoogopa kwenda kukopa benki kwa sababu taasisi hizo zimeanzishwa kwa ajili ya wananchi kukuza uchumi wao.

Akizungumza jijini hapa jana, katika hafla maalum iliyoandaliwa na NBC na kukutanisha wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa kutoka mikoa ya Kanda ya Ziwa ambao ni wanufaika wa benki hiyo, Kweka alisema alianza na mkopo wa Sh. milioni 17 mwaka 2005 sasa amefikia kiwango cha Sh. milioni 300.

Alisema baadhi ya wafanyabiashara hasa wanawake wamekuwa wakiogopa kukopa katika taasisi za kifedha hivyo kujikuta wanashindwa kukuza mitaji yao wakati ipo benki maalum iliyolenga kuwainua wafanyabiashara wa ngazi zote.

"NBC ni benki yetu wafanyabiashara tuitumie vizuri ili tunufaike nayo riba zake ni rafiki, mimi nilianza nikiwa mjasiriamali, lakini sasa ni mfanyabiashara wa kati, kikubwa ambacho nawasihi wafanyabiashara wenzangu ni uaminifu na kufanya biashara kwa kujituma ili kurejesha mkopo kwa wakati," alisema na kuongeza:

"NBC ni benki inayosikiliza wateja wake, binafsi nimenufaika sana kupitia benki hii, hata kipindi cha corona niliwafuata nikawaeleza kwamba sasa sijaagiza mzigo kutoka nje tukazungumza, wakanipunguzia riba kitendo hiki kinaonyesha kweli wamedhamiria kutuinua wafanyabiashara."

Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi, alisema lengo la benki hiyo ni kuhakikisha sekta binafsi inaendelea kupata sapoti ya kifedha kama mikopo na huduma za kibenki ili kuongeza uwezo wao wa kiuchumi na kukuza shughuli zao za uzalishaji hivyo kuwezesha uchumi wa nchi kuwa wa ushindani na kulifanya taifa kufikia uchumi wa kati.

Mkurugenzi wa Kitengo cha biashara kwa wateja wadogo na wakati kutoka NBC, Elvis Ndunguru, alisema lengo la kukutana na wafanyabiashara hao ni kuzungumza nao kuhusu bidhaa za kibenki ambazo benki hiyo inazitoa ili kuwawezesha wajasiriamali kukuza shughuli zao za kiuchumi.

"Leo tutawaeleza wafanyabiashara kuhusu bidhaa za mikopo tunazozitoa ambazo zimeondolewa dhamana kwa wafanyabiashara wanaofanya biashara na kampuni kubwa," alisema.

## Udhibiti panya kwa kutumia bundi kivutio Nanenane

**Na Ashton Balaigwa,** SIMIYU

TEKNOLOJIA ya kudhibiti panya waharibifu wanaoshambulia mazao katika mashamba ya wakulima kwa kutumia ndege aina ya bundi inayoonyesha katika Banda la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) katika maonyesho ya kilimo yanayofanyika kitaifa eneo la Nyakabindi mkoani Simiyu, imekuwa kivutio kikubwa kwa wakulima na wafugaji wanaotembelea maonyesho hayo.

Kivutio hicho kinatokana na watu kushangazwa na mnyama huyo ambaye pale anapoonekana, amekuwa akihusishwa na imani za kishirikina kutokana na uwezo wake wa kukamata panya anapokuwa shambani ambao wamekuwa adui wakubwa wa wakulima anapoonekana wakati sasa bundi ndiye rafiki wa mkulima.

Mhadhiri wa watafiti wa kituo cha kudhibiti viumbe hai waharibifu, Prof. Loth Mulungu, alisema njia inayotumika kwa ajili ya kudhibiti panya hao mashambani ni kujenga maboksi au masanduku pembezoni mwa shamba ambapo bundi atavutiwa na kuanza kutaga mayai katika eneo hilo.

Prof. Mulungu alisema masanduku hayo yanawekwa kwenye nguzo au miti pembezoni mwa mashamba na bundi anapoanza kufanya makazi katika eneo hilo chakula chake kikuu ni panya waliopo katika maeneo hayo na wakati wa kiangazi anatafuta ndani ya kilomita 4 na wakati wa masika anatembea eneo kubwa.

## 'Elimu dini dawa dhidi ya uhalifu'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAUMINI wa dini ya kiislamu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wametakiwa kuwasomesha watoto wao elimu ya dini itakayowafanya kuwa na hofu ya Mungu na kutoingia kwenye uhalifu hasa mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino watakapofika muda wa kujitegemea.

Hayo yalibainishwa jana na Shekhe wa Msikiti wa Ibadhi mjini hapa, Sulumu Hemed, wakati wa sherehe ya kuwalisha Eid Ali-Hajji wageni wa Jumuiya ya International Istiqaama Muslimu Community ya Oman iliyofanyika katika viwanja vya masjid Al-Wahaab Kata ya Nyasubi.

Alisema vijana wengi wanaingia kwenye matendo maovu kutokana na kukosa elimu ya dini na ya kujitegemea, ambapo wanapofika umri wa kujitegemea kimaisha hujiingiza katika matendo maovu yakiwamo mauaji ya vikongwe na watu wenye ualbino ambayo serikali imekuwa ikiyakemea kila siku.

Aidha, alisema kwa kiliona hilo, International Istiqaama imekuwa ikijenga misikiti mbalimbali kwenye maeneo ambayo hayana huduma hii ili kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuabudu na kuwa na hofu ya kutenda maovu.

Naye Katibu wa Masjid Ali-Wahaab, Ahmed Haroun, aliwataka wazazi na walezi kuacha ubaguzi wa kuwabagua watoto wa kike na kuwapeleka shule watoto wa kiume, huku wa kike wakiachwa kuendelea kusaidia kazi za nyumbani.




Ukurasa 13

Haijawezekana kuzikwa pamoja, wachongewe sanamu maalum

BUFE

IJUMAA AGOSTI 7, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

**Ofisa SUA: Biashara ya sungura inalipa nyama, kinyesi, mkojo**

# Ujangili unaofilisi tembo hifadhini na pigo la 'Operesheni Tokomeza'

- Miaka mitano waliuawa asilimia 60
- Leo wapya 80%; watuhumiwa 1,600

**Na Sabato Kasika**

WANYAMAPORI wana thamani na hilo linajulikana. Wachache kuwataja, kuna tembo, twiga, simba na nyati.

Hilo limewafanya majangili kuhangaika namna ya kuwapata na nyara zao, kwani wana thamani ya pesa, huku serikali nayo ikipambana kuwadhibiti wasidhuriwe, maana ni rasilimali na nyenzo ya uchumi wa taifa.

Wanaohitaji kuwashuhudia, kuna utaratibu maalumu kuwaingiza katika Hifadhi za Taifa, ambako kuna huduma zote za kuwezesha azima zao.

Katika vita dhidi ya ujangili, serikali ilibuni mbinu ya kuwafunga vifaa maalum, wanyama tembo katika hifadhi zao, ili kufuatilia na kukabili mwenendo wa majangili, maana azma hasi iliangukia katika tishio la wanyama hao kutoweka.

Tembo na wanyamapori wengine, wamekuwa kivutio vikubwa kwa utalii na kuliingizia taifa mapato na hasa katika fedha za kigeni, ambazo pale zinapoelekezwa katika uchumi, huzaa maendeleo ya nchi.

Watalii wamekuwa wakifika nchini kuwaona wanyama, kuwapiga picha na kuondoka, hivyo ni wazi wanyamapori wakiwamo tembo, wamebeba nembo ya utalii kwa kiasi kikubwa, inayoishia kusaidia uchumi wa nchi.

Aidha, hao tembo na orodha ndefu ya wanyama wanaojitokeza kwenye utalii wamefungua milango ya umma wa Watanzania kuajiriwa katika sekta za wanyamapori na utalii.

Hapo ndipo ilipobeba mtazamo wa serikali kuwa makini kukomesha ujangili kitaifa, ikiungwa mkono na wadau wengine.

**VITA UJANGILI**

Robert Mande, kamanda katika Kikosi cha Kuzuia Ujangili (NTAP), anaeleza mwaka 1961 wakati wa uhuru wa Tanganyika, kulikuwapo tembo 350,000 lakini miaka tisa baadaye 1970, ujangili ulishaanza kushika kasi. Mwaka 1980, hali ilikuwa mbaya.



Askari wanyamapori wakiwa katika nyendo zao ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.
**PICHA: MTANDAO**

Ni ufafanuzi aliyoutoa katika mkutano uliofanyika kwa njia ya mtandao ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira (JET) kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Marekani katika mradi wake wa 'USAID Protect'.

Anasema ndio mustakabali uliosukuma serikali mwaka 1989 kuanzisha operesheni maalumu iliyofanikiwa na hivi sasa NTAP kwa kushirikiana na wadau, inaendelea kuimarisha ulinzi wa usalama wa rasilimali hiyo ya utalii na mazingira kitaifa.

Kwa mujibu wa Mande, mafanikio kati ya mwaka 2018 na mwaka huu, asilimia 80 ya wanyama tembo wameongezeka maradufu.

**UJANGILI WASHAMIRI**

Mande anasema kati ya mwaka 2008 hadi 2013, ujangili dhidi ya wanyamapori ulishamiri zaidi, ukiwalenga tembo na inadaiwa wengi walivushwa kupitia bandari za pande zote, Bara na Visiwani.

"Mwaka 2009, tembo waliongezeka na kufikia 109,051, lakini 2013 ujangili uliongezeka na (mwaka) 2014 idadi yao ilipungua hadi kufikia 43,000 ikiwa ni sawa na asilimia 60 ya tembo wote waliokuwapo nchini, hali iliyoifanya serikali kuanzisha Operesheni Tokomeza," anasema Mande.

Mande anasema ishara ya kuingezeka ujangili, mwaka 2014, serikali ilianzisha NTAP kwea kushirikisha vikosi vya ulinzi na usalama, idara za wanyamapori na taasisi nyinginezo na mwaka 2016 wakaanza kutekeleza.

"Kwa mwaka 2015 hadi 2020, NTAP tulikamata tani 10,000 za mbao, risasi 25,000, wanyama waliokuwa hai 2,000, watu 3000 waliokuwa wakijihushisha na mtandao wa ujangili walichunguzwa na kukamatwa," anasema.

Anafafanua katika kundi hilo, kuna watu 2000 walifikishwa mahakamani na 300 walibainika kuwa vinara wa ujangili, wakijumuisha watokao nje ya nchi.

Pia, anasema watuhumiwa 1,600 wa ujangili walihukumiwa vifungo kati ya miaka 10 na 20 na wengine 43 walilipa faini jumla ya shilingi bilioni mbili, akidokeza walichogundua, ujangili unafanyika kwa njia ya mtandao, hifadhini pamoja na mijini.

"Naweza kusema kwamba, ujangili umepungua nchini kwa asilimia 80 na inawezakana ikawa zaidi ya hapo," anasema Mande, huku akijivuna kwamba idadi ya tembo nchini hivi sasa inaongezeka.

**WASHIRIKA**

Salimu Msemo, Ofisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS), anasema wanashirikiana na taasisi mbalimbali za kuserikali, zikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Idara ya Uhamiaji.

Wengine wanaosikitikiana na wadau wakuu, NTAP, anatawaja kuwa ni maofisa wanyamapori, vyombo vya habari na vingine vya ulinzi na usalama.

"Makosa ya ujangili yamechangia wahusika kutaifisha magari, nyumba na mali nyingine zilizotokana na ujangili wa wanyamapori au misitu, na kuwafanya wananchi waogope kujihusisha na vitendo hivyo," anasema Msemo.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, anasema, mkakati wao ni kuendelea kufunza wanahabari kuhusu utunzaji mazingira, utalii na ujangili wa wanyamapori kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

BIASHARA

# Ofisa SUA: Biashara ya sungura inalipa nyama, kinyesi na mkojo

## • Hili hapa darasa la anavyofugwa
## • Ajigamba wana 'Muhimbili' yao

**Na Christina Haule, MOROGORO**

UFUGAJI sungura umekuwa ukifanywa na watu wachache duniani, wengi wakiichuku katika namna ya mapambo na kujifurahisha.

Hyasinta Minde, Ofisa Mifugo kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA), anaeleza faida za ufugaji sungura kuwa ni wanyama wanaoweza kusogeza mbele mnyororo wa thamani na kuongeza kipato kwa wafugaji.

Anasema, mbali na yake kubwa, pia mfugaji ananufaika kwa kuuza mkojo wake ambao ni dawa ya kuua wadudu kwenye mboga na matunda.

Minde anataja faida nyingine ya ufugaji sungura, ni kuweza kufuga idadi kubwa apendavyo na kuweka vifaa vya kutegea mkojo anaouhifadhi kwa usafi, kisha baadaye anahamishia kwenye chupa, tayari kuwasilishwa sokoni iuzwe kukidhi mahitaji mengine.

Kwa mujibu wa Minde, hivi sasa kila lita ya mkojo wa sungura, inauzwa kwa bei ya shilingi 10,000 na kinyesi cha mnyama sungura ni bidhaa ya kufanyiwa biashara, kwani kinauzwa kwa shilingi 250 kwa kilo.

Minde anasema, sungura anaweza kuuzwa kwa bei inayoendana na mazingira ya ubora wake na soko aliko.

Anataja baadhi ya aina za sungura, wakiwamo California White, German Giants, Newsland White, American Sports, Angola, Kutch na Chinchilla, ambao wanapatikana kwa wataalamu wa SUA kwa sasa.



Ofisa Mifugo, Hyasinta Minde, akionyesha sungura waliopo kwenye banda la Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), kwenye Maonyesho ya Wakulima '88' Kanda ya Mashariki, mjini Morogoro. **PICHA : CHRISTINA HAULE.**

### MIMBA ZAO

Ofisa huyo anasema, sungura anabeba mimba kwa wastani siku kati ya nane na 35 ndani ya kipindi hicho anazaa watoto wasiopungua wanane hadi 12 kwa uzao mmoja.

Pia, anasema kuna kawaida sungura anaweza kuzaa mara tano kwa mwaka, hivyo mfugaji kunufaika na wastani wa sungura 40, mlo mkuu ukiwa ni pumba na maji na ukuaji wao huchukua kati ya miezi minane hadi kuwa tayari kuliwa.

Minde anaeleza kuwa hiyo sifa ni kwa aina ya mbegu zote, iwe ya kizungu (broiler) au ya kienyeji na nyama yake inafanana na ya kuku, ambayo ni sehemu ya nyama nyeupe inayofaa kiafya na kumuongezea mlaji protini mwilini.

Ili akue katika mazingira salama, Minde anasema inashauriwa sungura awekwe mbali na mazingira ya majimaji wakati katika mabanda anakoishi, ambako kunapaswa kuwa juu na kuna sehemu ya chini ya kushusha mkojo na kinyesi.

### MATIBABU YALIVYO

Minde anataja kuwapo ugumu wa kumfuga mnyama sungura, ambao ni pamoja na magonjwa ya kuhara damu, minyoo ya ngozi, lakini yanatibika katika maeneo ya tiba ya wanyama, hali kadhalika maduka ya dawa mahsusi kwa mifugo.

Hata hivyo anasema mkojo wa sungura kama dawa ya kuua vijidudu waharibifu wa mboga na matunda hauleti madhala kama mtumiaji atatumia kwa kufuata ushauri anaopewa.

Isaack Kashoma, Daktari Mkuu wa Hospitali ya Wanyama SUA, anasema kituo hicho cha matibabu ni kikubwa na maalum kwa ajili huduma kwa wanyama aina zote, wasiofugwa na walioko porini.



Matunzo ya sungura ndani ya banda la kisasa. Picha nyingine kulia juu, sungura wakiwa bandani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Katika mahali hapo panafanyika vipimo na ugunduzi wa magonjwa yanayosumbua wanyama, matibabu yao, chanjo na ushauri.

### HOSPITALINI SUA

Anasema hospitali ya wanyama SUA ni ya kipekee ya rufani ya kwanza mahsusi kwa wanyama, iliyoanzishwa mwaka 1984, chuo kilipoanzishwa.

Iliboreshwa zaidi kwa kuwekewa vifaa maalum kuanzia mwaka 2015, ikiendelea kuboreshwa kwa sasa ili kila kitu kinachotakiwa kwa ajili ya ugunduzi wa magonjwa kwa wanyama kiwepo.

Dk. Kashoma anasema, wanyama aina ya sungura, nguruwe, ngamia na wengine wanawahudumia kitiba pale wanapokuwa na magonjwa.

Anasema, pia wanatoa huduma za matibabu mbalimbali kwa mbwa ambapo kuna chanjo za kichaa cha mbwa wanaendelea kutoa kwenye hospitali hiyo, pamoja na kukabili magonjwa mbalimbali.

Hapo anayataja magonjwa ya kuharisha, kutapika na homa ya manjano, ambayo kwa sasa ni wastani wa mbwa 50 kila wiki wanapatiwa chanjo dhidi ya magonjwa hayo kutoka mkoa wa Morogoro.

Aidha, anasema pia wamekuwa wakitoa huduma kwa wanyama wagonjwa kutoka mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es salaam, Tanga, Dodoma, Iringa na Pwani kwa huduma za mbwa wanaopelekwa kwa huduma za rufani.

Hiyo inajumuisha waliovunjika sehemu za miili yao na wanauhitaji kufungwa, wenye uvimbe sehemu na wahitaji wa x-ray, Dk. Kashoma anasema wote wana nafasi ya kuungwa katika matibabu hayo hospitalini SUA hapo na kuondoka wakiwa na afya njema.

Awashauri wakulima kutambua kwamba ufugaji wanyama una faida kubwa, hivyo wajenge tabia ya kuwapenda na wasisite kuwapelekea hospitalini SUA wanapoumwa.

Rai yake ni kwa wakulima watembele banda la SUA kupata ushauri wa masuala kitaalamu kuhusu mifugo katika maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima '88' katika banda lao.

Dk. Kashoma anasema, pia watatumia fursa hiyo kutoa huduma ya bure ya chanjo dhidi ya kichaa cha mbwa, ingawa anakiri kuwapo ugumu katika kuwafikia wanyamapori.

Ili kufanikisha namna ya kuwafikia wanyama wakali porini kutibiwa, nataja mbinu kwamba endapo miundombinu au njia maalum ya kuwafikia itaandaliwa vizuri, wanaweza kuwapata kwa wanyama hao na kuwahudumia vyema na hivyo kuendelea kukuza rasilimali za Taifa.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Haijawezekana kuzikwa pamoja, wachongewe sanamu maalum






**NA JOSEPH KULANGWA**

MUNGU aliumba dunia kwa namna alivyojua yeye, aliumba binadamu kwa mfano wake na kumpa muda maalumu wa kuishi katika dunia hiyo. Baada ya binadamu kumaliza muda wake wa maisha duniani, zipo imani kwamba hutwaliwa na Mungu huyo huyo.

Lakini, katika kutwaliwa huko, inaaminika pia kuwa Mungu huchukua roho ya mhusika na kuacha kiwili wili kuhifadhiwa na binadamu wenzake.

Hivyo wapo marehemu ambao huzikwa na wengine huchomwa moto. Wanaozikwa huhifadhiwa makaburini.

Zamani kabla ya teknolojia, wafu walichimbiwa mashimo, yakaitwa makaburi na kuzikwa ama bila nguo au kwa kuviringishiwa nguo, majani au hata ngozi, ili mradi walikaa makaburini kwa muda fulani waliozaa, kugeuka udongo na kukidhi kauli ya 'ulitoka mavumbini na utarudi mavumbini'.

Leo baada ya teknolojia, binadamu (baadhi) wanazikwa wakiwa kwenye masanduku maalumu, majeneza, huku makaburi yakijengewa marumaru. Lakini dhana yote inabaki ileile, ya 'kutoka mavumbini na kurejea mavumbini.' Makaburi ama huwekwa alama au yanajengewa kwa ajili ya kumbukumbu na hata matambiko.

Zipo serikali duniani ambazo zimekuwa na utaratibu wa kuhifadhi viongozi wao wanapokuwa wameaga dunia. Tanzania ni mojawapo, ambayo kisheria imekuwa na kifungu hicho.

Na kwamba iliamuliwa kwa mujibu wa sheria hiyo, kwamba viongozi wakuu wa nchi wakifariki dunia, basi wazikwe Dodoma yaliko makao makuu ya nchi.

Eneo lilishatengwa, lakini wahusika wamekataa kuzikwa hapo. Hiyo ilithibitishwa mnamo Julai 28 wakati wa mazishi ya kitaifa ya Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, kwamba viongozi walengwa wamekataa na badala yake wametaka wazikwe kwao, vijijini walikozaliwa.

Hiyo inafuata nyayo za Baba waTaifa Mwalimu Julius Nyerere, ambaye alizikwa kijijini kwao Butiama, mkaoni Mara.

Akithibitisha kukubaliwa kinadharia kwa sheria hiyo na baadaye kukataliwa kivitendo, Rais Dk. John Magufuli, aliwaambia Watanzania kuwa Mkapa alisema atazikwa Lupaso, Jakaya Kikwete akasema yeye azikwe Msoga mkoani Pwani na yeye Magufuli azikwe Chato mkoani Geita.

Alipoona wote wamekataa akiwamo yeye, akaona ni bora eneo lililotengwa sehemu yake warejeshewe wananchi kwa shughuli zao za maendeleo na sehemu iliyobaki, ikitokea Waziri Mkuu mstaafu John Malecela amefariki dunia, basi itumike kumzika kwa sababu Dodoma ni kwao.

Anasema alichelea kumuuliza Mzee Ali Hassan Mwinyi, akiamini naye asingekubali ombi hilo.

Hii maana yake nini, pengo la kihistoria? Wazo la kutenga eneo maalum kwa ajili ya maziko ya viongozi wa kitaifa lilikuwa na maana ya kuweka historia na kumbukumbu kwa vizazi vijavyo, lakini lingekuwa ni eneo la utalii.

Fikiria eneo lenye makaburi ya Nyerere, Mwinyi, Mkapa, Kikwete, Magufuli na wengine watakaofuata panapo majaliwa na Mungu, linakuwa na kivutio gani kwa wanafunzi wa historia ya kitaifa, pia watalii wa ndani na nje ya nchi?

Ni dhahiri hiyo fursa haitakuwapo tena, kwa sababu haitarajiwi kirahisi kuwa atakuja kutokea kiongozi mkuu wa nchi, atakayeamua vinginevyo siku zijazo na kuhamisha makaburi kutoka Butiama, Unguja, Lupaso, Msoga, Chato na kwingineko, kuletwa Dodoma kwa ajili hiyo.

Basi kwa kuwa ni hivyo na kwa kuwa historia, bado ni muhimu na makumbusho bado yanahitajika, linaweza kufanyika kitu kingine mbadala. Litafutwe eneo lingine tena, ambako kutajengwa sanamu za maarufu hao, ambazo zitaishi kwa muda mrefu kwa manufaa ya kihistoria.

Wapo wataalamu waliobobea katika fani hiyo, wanaoweza kuchonga/kujenga sanamu nzuri na za kuvutia, lakini zinazofanana hasa na wahusika, ili hata kizazi kijacho kikiziona basi kijisikie kuwa kilipata kuijua sura ya Nyerere, Mwinyi, Mkapa, Kikwete au ya Magufuli na watakaofuata baadaye.

Kupanga na kuchagua. Tusipofanya hivyo na kuendelea kufungua makumbusho katika kila kijiji alichozaliwa Rais, haitakuwa rahisi.

Pia ni vigumu watu kufanya safari za kwenda katika kila kijiji husika kuona sura za maarufu hao na kazi walizofanya. Kituo kimoja ni mwafaka kabisa. Alamsiki!

• Simu: (+255) 713 410008
na baruapepe:
jkulangwa@yahoo.com

UCHUMI

# Mlipuko bandarini waipa Lebanon dhiki kuu, haijui mahali ijikwamue

- Akiba ya ngano kitaifa 'nyang'anyang'a
- Wakubwa watolea macho, shida siasa
- Yawakuta dola bei 1500, mpya 8000



Ndivyo ilivyo athari za mlipuko katika Bandari ya Beirut, nchini Lebanon, Jumanne wiki hii. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

UCHUMI wa nchi ndogo ya Mashariki ya Kati yenye machafuko na vita vya miaka mingi, Lebanon, umeingia shakani zaidi, baada ya mlipuko mkubwa wa kemikali kama bomu katika bandari ya Beirut, jioni siku tatu zilizopita.

Ni adha iliyosababisha watu 135 waliotambuliwa kufariki mapema na zaidi ya 4000 wanahitaji matibabu. Wengine bado walikuwa ama hawajaokolewa au kufukuliwa kutoka majengo yaliyoanguka na vifusi vilivyotapakaa, hasa vya madirisha ya vioo.

Ni mlipuko unaoongezea mzigo kwa uchumi uliokuwa taabani. Moja ya athari za awali za mlipuko huo ni kuteketezwa kwa Hifadhi ya Ngano ya nchi hiyo, iliyokuwa katika maghala ya zege bandarini hapo, iliyoharibiwa kabisa.

Takwimu za kiserikali za Marekani zilionyesha kuwa asilimia 80 ya mahitaji ya ngano nchini humo yanategemea kuagizwa kutoka nje.

Aidha, inafafanuliwa kuwa asilimia 85 ya ngano tarajiwa (ambayo inaelekea ilitazamiwa kutumia muda mrefu kiasi) ilikuwa katika maghala hayo ya bandarini.

**CHANZO MLIPUKO**

Mlipuko wenyewe uliotokana na hifadhi ya tani 2,750 za bidhaa malighafi ya kemikali ya 'ammonium nitrate' ambayo mara nyingi inatumika kutengeneza mbolea, hata mabomu.

Hiyo inafanya hali iwe ngumu zaidi kukabiliana na uhalisia, baadhi ya hospitali muhimu jijini Beiruit ziliathirika na mlipuko huo, ambao unafanana na bomu la kihistoria la atomiki nchini Japan.

Siku ya Agosti 4 ni mkesha wa kuamkia kuangushwa kwa bomu la Hiroshima na punde bomu lingine Nagasaki, iliyokuwa kwenye miji yenye viwanda vingi vya vifaa vya kijeshi.

Mabomu hayo yalimaliza vita kati ya Marekani na Japan wakati wa Vita Kuu ya Pili, ikaielekeza nchi hiyo kukataa kutengeneza mabomu ya nuklia.

Hata hivyo, kuhakikisha misaada kwa Lebanon haielekei kuwa ni kazi rahisi, kwani imezungukwa na nchi zilizoko ama vitani au zenye uhasama na baadhi ya makundi ya siasa na kijamii nchini Lebanon.

Syria ndiyo jirani wa karibu zaidi na iko vitani 'kivyake' wakati Israel 'haiivi'na kundi la Hezbollah, lenye nafasi muhimu katika jamii ya Lebanon. Inabakiza kuwa kitendawili.

**WAKUBWA WAJISOGEZA**

Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa, alianza maandalizi ya kufika nchini humo siku mbili baada ya mlipuko, kuangalia kwa karibu hali ilivyo na nini kinaweza kufanyika.

Ufaransa ilitawala nchi hiyo kwa miongo kadhaa wakati wa kuanguka kwa himaya ya Kituruki wakati wa Vita Kuu ya kwanza barani Ulaya na imeendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Lebanon.

Ilikuwa tayari inaandaa kupeleka wataalamu wa misaada katika maeneo tofauti kuanzia uokoaji, tiba au kwingine, pia tani kadhaa za misaada ya kibinadamu inayohitajiwa haraka.

> **"Hiyo inafanya hali iwe ngumu zaidi kukabiliana na uhalisia, baadhi ya hospitali muhimu jijini Beiruit ziliathirika na mlipuko huo, ambao unafanana na bomu la kihistoria la atomiki nchini Japan.**

Eneo la upatikanaji nafaka baada ya kuungua maghala hayo bandarini, lilikuwa ni tatizo zaidi na lilikuwa halijaanza kujadiliwa kwa kina.

Hata hivyo, Marekani ndiyo inayochangia kwa kiasi kikubwa katika shughuli za Shirika la Umoja wa Mataifa la Misaada ya Chakula (WFP), ila kuna tatizo.

Mtazamo upo kwamba Marekani itakapotoa misaada hiyo, itabidi ihakikishe haitaingia mikononi mwa kundi la Hezbollah, kuifanya asilimali mpya.

Nje ya jitihada hizo za Ufaransa, Umoja wa Ulaya (EU) ikiwa ni mkusanyiko wa taasisi na mataifa, ulikuwa inaandaa wafanyakazi wa kutoa huduma za dharura na vifaa kutoka nchi zote 27 wanachama.

Hiyo ina maana kuwa, siyo taasisi iliyoko wima ambayo ingefanya kazi hiyo, ila kupitisha michango kutoka eneo lote hilo inayokidhi kiasi fulani mahitaji ya jirani huyo wa Ulaya.

Nchi yenye nguvu zaidi ni China, na ilikuwa tu imepeleka salamu za rambirambi bila ya kutaja mpango wowote, ila bila shaka inafikirika.

**DIPLOMASIA MPYA?**

Kwa upande mwingine, mlipuko huo unaelezwa unaweza kubadili haraka mwelekeo wa 'Diplomasia ya Uchumi' nchini humo, kutokana na serikali na makundi tofauti ya kisiasa, kutokuwa tayari kuafikiana na mashirika ya fedha ya kimataifa kama IMF na Benki ya Dunia.

Tayari kuna miito iliyosikika kuomba ushirikiano wa karibu zaidi na China, inayohusika katika kuboresha miundombinu nchini humo kwa miongo takriban miwili sasa.

**NAFASI YA CHINA**

Wachunguzi wa habari nchini Marekani wansema, China inapendelea Lebanon ijiunge na mpango uitwao 'Belt and Road Initiative' (ukanda na barabara, yaani ukanda wa biashara, hivyo kufufua reli ya kati ya Beirut na Tripoli, ufukwe wa Bahari ya Kati.

Licha ya mipango hiyo ndiyo, awali ilianza kujadiliwa, wachunguzi wanauona kuwa mtego unaozuka, kutokana na kuungua kwa bandari ya Beirut katika mlipuko.

Suala hapo linatajwa kuimarishwa bandari na kupewa mkataba wa kuiendesha, ili irudishe gharama zake na kupata faida ni moja ya programu za kawaida ambazo China inapendekeza kwa nchi zinazoshiriki katika mipango yake.

Hiyo iko tofauti na utoaji mikopo na riba kubwa, ili nchi ishindwe kulipa halafu ianze kubinafsisha benki zake.

Hata hivyo, siyo wataalamu wote au wengi nchini Lebanon wanaoona kuwa msaada muhimu utatoka China, kwa msingi kuwa mwelekeo wa China hasa ni kwenye kuimarisha miundombinu, wakati Lebanon inahitaji misaada mikubwa ya fedha ili itoke katika mkwamo wa sarafu.

Miezi kadhaa iliyopita, sarafu ya Lebanon (dinari) ilikuwa inabadilishwa kwa kila dola moja ya Marekani, ilinunuliwa kwa dinari 1,500 kwa.

Lakini, mwanzo wa mwezi huu, dola moja sasa inauzwa kwa dinari 8,000 katika soko 'mbadala.' Wengi kati ya wataalamu wa Lebanon, wanataka nchi hiyo iingie katika majadiliano ya kina na IMF.

Hivyo, kutokana na mkasa huo, hitaji la kuitegemea Ufaransa na Umoja wa Ulaya kunatarajiwa kuiweka China mtegoni, kama ina uwezo wa kutoa pendekezo toshelevu kusaidia kuikwamua Lebanon katika mkasa, isitegemee kukubaliana na nchi za Magharibi.



# Migogoro ya ardhi yatatuliwa kwa 80%

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema kwa kipindi cha miaka mitano wamefanikiwa kutatua migogoro sugu ya ardhi kwa asilimia 80.

Kunambi, aliyasema hayo jana jijini hapa, wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya Jiji la Dodoma katika kutatua migogoro ya ardhi.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano jiji hilo limefanikiwa kuondoa kero ya migogoro sugu ya ardhi ambayo ilikuwa inawakabili wananchi wa meneo mbalimbali.

Mafanikio hayo alisema kwa kiasi kikubwa ni juhudi na uwajibikaji mkubwa kutoka kwa watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kuwatumikia wananchi wake kwa hali na mali. Kadhalika, wamegawa viwanja 3,044, kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miradi mbalimbali iliyokuwa ikitekelezwa katika maeneo yao.

Alisema kuwa Jiji la Dodoma linakua kwa kasi kutokana na juhudi za Rais John Magufuli kutoa fedha za kutekeleza miradi mikubwa yenye hadhi ya jiji la kimataifa.

"Miradi hiyo ni soko kuu la Ndugai, kituo kikuu cha mabasi, kituo cha maegesho ya malori na magari makubwa, mtandao wa barabara na sehemu ya kupumzika yote ikiwa na thamani ya Sh. bilioni 89," alieleza Kunambi.

Vilevile, soko la Ndugai limetumia Sh. bilioni 14.6, stendi kuu ya mabasi Sh. bilioni 24, sehemu ya kupumzika (Chinangali Creation Center), Sh. bilioni 2.9 na mtandao wa barabara ukitumia Sh. bilioni 26.7.

Alitoa wito kwa wakazi wa jiji hilo kutoa ushirikiano wa kutosha ili kuendelea kusukuma maendeleo pamoja na kutunza miundombinu iliyotumia kiasi kikubwa cha fedha za umma.




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Mkumbo Myonga, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa simu ya Infinix hot 9, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Meneja Uhusiano wa Infinix, Saiphon Asajile. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Watoto wenye ulemavu wasikatishwe ndoto kielimu'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

OFISA Miradi ya Elimu Jumuishi kitengo cha kanisa la Free Pentecostal of Tanzania (FPCT), Wilaya ya Dodoma na Bahi mkoani Dodoma, Jane Mgidange, amewataka wazazi na walezi kutozima ndoto za watoto wenye ulemavu kwa kushindwa kuwaendeleza kimasomo.

Mgidange, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na wazazi na walezi, ambao familia zao zina watoto wenye ulemavu wanaosoma katika kata ya Nkuhungu.

Alisema watoto wenye ulemavu wana haki ya msingi ya kuendelezwa ndoto zao kimasomo badala ya kuwaficha na kuwaweka majumbani.

Kuna baadhi ya wazazi na walezi, alisema hawana moyo wa kuwaendeleza watoto hao wenye ulemavu, kwa imani kuwa hawawezi kutoa mchango wowote kwenye jamii wanayoishi suala ambalo ni upofu wa fikra.

"Changamoto iliyopo kwa wazazi na walezi wenye watoto wenye ulemavu, wanawaona watoto hao kama ni sehemu ya mkosi hivyo hakuna haja yoyote ya kuwaelimisha kimasomo japo kuwa wengine wana vipawa," alisema.

Recho Lauret (11), mwenye ulemavu wa viungo mwanafunzi wa darasa la tano, Shule ya Msingi Nkuhungu, alisema changamoto waliyonayo ni ukosefu wa vifaa rafiki visaidizi na kutembea mwendo mrefu kuifuata shule.

Alisema, kutokana na ukosefu huo wa vifaa rafiki kunasababisha wenye ulemavu wengi kushindwa kufikia ndoto zao.

# Wenye utapiamlo wazidi kuibuliwa Dodoma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

HALMASHAURI za Mkoa wa Dodoma, zimeongeza kiwango cha uibuaji wa watoto wenye utapiamlo kufikia asilimia 79, katika kipindi cha Juni 2020, kutoka asilimia 11, Desemba 2019.

Mratibu wa Lishe Mkoa wa Dodoma, Herieth Carin, alibainisha hayo jijini hapa katika kikao cha tathmini ya hafua za lishe katika halmashauri za mkoa.

Alisema halmashauri nyingi, zimetekeleza mkataba wa lishe katika kipindi cha nusu mwaka kati ya Julai hadi Desemba 2019.

"Halmashauri zimeongeza kasi ya uibuaji watoto wenye utapiamlo mkali kwa watoto wa chini ya miaka mitano na kutoa matibabu kwa watoto hao," alisema Carin.

Alisema halmashauri hizo zilitoa mafunzo ya matibabu ya utapiamlo mkali kwa watoa huduma za afya 223, wakiwamo 155 kutoka wilaya za Mpwapwa, Kongwa (21), Chamwino (19), Bahi (5), Dodoma Jiji (12), Chemba (2), Kondoa (3) na Kondoa Mji (5).

Kadhalika, halmashauri zilifanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa takwimu kwa kuandaa na kusambaza fomu maalumu za kukusanyia taarifa kwa wahudumu ngazi ya jamii pamoja na vituo vya kutolea huduma.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya halmashauri zilitoa fedha kidogo tofauti na zilivyotenga kwenye bajeti yake kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe, ili kupunguza athari za kilishe kwa watoto hao.

Kati ya halmashauri hizo, alisema Chamwino iliongoza kwa kutenga na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya afua hiyo kwa kutenga Sh. milioni 22.4 na kutumia Sh. milioni 22.3 sawa na asilimia 99, ya fedha hizo.

"Halmashauri ya Bahi, ilitenga Sh. milioni 54.5 na ikatumia milioni 44.6 sawa na asilimia 82, wakati Mpwapwa ilitenga Sh. milioni 72.1 na ikatumia Sh. milioni 55.3, sawa na asilimia 78.

"Halmashauri ya Kondoa Mji ilitenga Sh. milioni 32.3, lakini ilitumia Sh. milioni 19.02 sawa na asilimia 59, wakati Kongwa ilitenga Sh. milioni 86.8 na kutumia Sh. milioni 50.02 sawa na asilimia 58 ya bajeti.

"Kondoa ilitenga Sh. milioni 76.2, lakini ikatumia Sh. milioni 30.7 sawa na asilimia 40, wakati Jiji la Dodoma lilitenga Sh. milioni 147.03, likatumia Sh. milioni 54.7 sawa na asilimia 37, vilevile Chemba ilitenga Sh. milioni 53.5 ikatumia Sh. milioni 11.5 sawa na asilimia 21," alifafanua.

Alisema halmashauri kupitia idara zake mtambuka za lishe zikiwamo idara ya maendeleo ya jamii, elimu, kilimo na ufugaji ziliendelea kutoa elimu kwa jamii namna bora ya kuinua na kuongeza kipato katika ngazi ya kaya.

Alieleza kuwa kwa kutumia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na mifuko ya vijana na wanawake halmashauri zilipata fedha za kuinua hali zao za lishe.

Pia kupitia idara hizo yalitolewa mafunzo ya kilimo cha mboga na ufugaji wa wanyama wadogo katika halmashauri za Bahi, Mpwapwa, Kongwa, Chamwino, Dodoma Jiji, Kondoa, Kondoa Mji na Chemba.

"Mafunzo hayo yalitolewa kwa wahudumu wa afya ngazi za jamii 906, kutoka Bahi, Chamwino, Chemba, Mpwapwa, Kongwa, Kondoa na Kondoa Mji kwa kushirikiana na wadau wa Lishe Endelevu, Lishe Dodoma, Boresha Lishe na World Vision," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, aliwapongeza wakurugenzi ambao walitenga fedha katika bajeti zao na kutumia kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe kwa asilimia kubwa.

Shekimweri, aliwataka wakurugenzi ambao walitenga fedha, lakini hawakutumia kwa ajili ya afua hiyo, kufanya hivyo kwa lengo la kuendelea kupunguza athari za utapiamlo miongoni mwa watoto wa chini ya miaka mitano.





## Taasisi yagawa mbegu bure

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imegawa bure mbegu za baadhi ya mazao kwa wananchi wanaotembelea banda la taasisi hiyo kujifunza mbinu bora za kilimo kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ili kuwahamasisha kutumia mbegu bora.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema juzi kuwa mbegu ambazo wanagawa kwa wakulima ni maharage ya aina tofauti ambayo yamefanyiwa utafiti kwenye kituo hicho na kwamba lengo ni kuwashawishi wakulima kutumia mbegu hizo kwenye msimu ujao wa kilimo.

Alisema mbegu za maharage ambazo taasisi hiyo imewagawia wakulima zina faida kubwa kiuchumi na kiafya kutokana na kuhitajika zaidi kwenye soko.

Dk. Bucheyeki alisema baadhi ya maharage hayo ni kwa ajili ya lishe na yana virutubisho ambavyo vinahitajika kwa ajili ya kukabiliana na udumavu wa watoto ambao ndio tatizo kubwa kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

"Tunagawa gramu 100 kwa kila mkulima ambaye anatembelea banda letu na kwenye mashamba darasa kuja kujifunza kilimo bora cha mazao haya. Lengo letu ni kuhakikisha wananchi wanahamasika kutumia mbegu bora," alisema Dk. Bucheyeki.

Alisisitiza kuwa wakulima wa mikoa hiyo wanatakiwa kuachana na kilimo cha mazoea na badala yake wazalishe kibiashara kwa kutumia mbegu bora ambazo zimefanyiwa utafiti na kufuata maelekezo ya wataalamu wa kilimo.

Kilimo, alisema ni miongoni mwa sekta ambazo zimeliwezesha taifa kuinuka kiuchumi na kufikia uchumi wa kati na hivyo akasisitiza kwamba endapo sekta hiyo itaimarishwa zaidi kuna uwezekano wa taifa kupiga hatua zaidi.

Dk. Bucheyeki alisema mbali na kugawa mbegu hizo pia wataalamu wa taasisi hiyo wameendelea kutoa elimu ya kilimo cha mazao mbalimbali ya biashara na ya chakula ili wananchi waongeze uzalishaji utakaopelekea taifa kujitosheleza kwa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje.

Aliyataja baadhi ya mazao ambayo wananchi wanafundishwa kulima kuwa ni pamoja na mahindi, maharage, ngano, ulezi, mpunga, viazi lishe, alizeti, maparachichi na pareto na kwamba zipo teknolojia zaidi ya 50 ambazo taasisi hiyo imebuni na inazisambaza kwa wananchi.

# SAUT Mbeya sasa Chuo Kikuu Kishiriki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), imekipandisha hadhi kilichokuwa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) Kituo cha Mbeya, kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya (CUCoM).

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi rasmi wa chuo hicho, Rais wa Baraza la Maaskofu Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) , Askofu Gervas Nyaisonga, alisema chuo hicho kilipata sifa ya kupandishwa hadhi baada ya kutimiza vigezo vilivyokuwa vinahitajika.

Alisema Kanisa Katoliki litaendelea kushirikiana na serikali katika uboreshaji wa elimu ya juu ili kuliwezesha taifa kuwa na wasomi wengi ambao watakuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya ndani na nje ya Tanzania.

Askofu Mkuu Nyaisonga ambaye ndiye Mkuu wa Kwanza wa CUCoM, alisema sekta ya elimu nchini bado iko nyuma ikilinganishwa na ukubwa wa nchi pamoja na mahitaji ya wananchi hali ambayo alisema inawafanya baadhi ya wananchi kushindwa kutatua shida zao kitaalamu.

Kwa mujibu wa Askofu Mkuu Nyaisonga, ukosefu wa idadi kubwa ya wasomi wenye uwezo wa kusimamia rasilimali za taifa na kutatua matatizo ya wananchi, ni sawa na kondoo waliokosa mchungaji, hivyo wanatangatanga na kuzurura ovyo.

"Kuna watu wanaweza wakawa wanajiuliza maswali kwamba kwa nini kanisa liendelee kujenga vyuo vikuu wakati vipo vingi nchini? Na je, kanisa litaendelea kujenga hivyo vyuo? Jibu ni kwamba kwa hadhi na ukubwa wa nchi yetu, bado tunahitaji wasomi wengi wa elimu ya juu ambao watakuja kujibu haja za Watanzania, hivyo tutaendelea kujenga vingi zaidi," alisema Nyaisonga.

Akizundua chuo hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema serikali kwa kutambua mchango wa vyuo vikuu katika nyanja za kijamii na kiuchumi, inao wajibu wa kuhakikisha inaweka miundombinu mizuri itakayowawezesha wanafunzi kujisomea bila shida.

Chalamila alisema serikali itahakikisha huduma za kijamii kama maji na umeme zinapatikana kwa uhakika katika maeneo yote ya kutolea elimu ili kuhakikisha sekta hiyo inakua kwa kasi na kuzalisha wataalamu.

"Katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST), tumejenga barabara yenye urefu wa kilomita 2.8 ili kurahisisha usafiri. Lakini hapa nipo na Meneja wa TARURA (Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini) , Injinia Matindi, nadhani atafanya utaratibu wa 'ku-connect' (kuunganisha), kababarabara haka na lami ili kaingie vizuri zaidi hapa chuoni," alisema.

Makamu Mkuu wa SAUT, Balozi Prof. Costa Mahalu, aliahidi kuendelea kushirikiana na idara zote zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kuendelea kutoa elimu bora kwa Watanzania.

Prof. Mahalu alisisitiza kuwa kwa sasa Tanzania inahitaji elimu bora kwa wananchi ili kuzalisha wataalamu watakaoziinua sekta mbalimbali na kuimarisha uchumi wa nchi.

Aliwataka Watanzania kuchangamkia fursa ya kuwapeleka watoto wao kwenye vyuo vikuu ndani na nje ya nchi ili wapate utaalamu utakaowawezesha kulisaidia taifa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.



Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Gelvas Nyaisonga (kushoto), akifurahia jambo na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, baada ya kukamilika kwa uzinduzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Kikatoliki cha Mbeya (CUCoM), ambacho kimetokana na kupandishwa hadhi kwa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino (SAUT) Tawil la Mbeya, mapema wiki hii. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali yatoa elimu uzalishaji kuhusu malisho bora ya mifugo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeanza kutoa elimu ya utunzaji wa malisho na kugawa mbegu za malisho bora ya mifugo kwa wafugaji wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ili kuepuka kuzorota kwa ubora wa mifugo hasa kipindi cha kiangazi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) Kituo cha Mbeya, Dk. Edwin Chang'a, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya idara mbalimbali za Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye Maonyesho ya Wakulima (Nanenane) kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini hapa.

Alisema wakati wa kiangazi, wafugaji wa mikoa hiyo hukabiliwa na upungufu wa malisho bora, hivyo kusababisha ubora wa mifugo pamoja na mazao yake kupungua na wakati mwingine baadhi ya maeneo mifugo hufa.

Alisema TALIRI kwa kushirikiana na idara zingine zikiwamo Wakala wa Ranchi za Taifa, na idara ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo, wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kwa njia mbalimbali ili kuepuka matatizo hayo.

"Sisi tunazalisha na kusindika malisho ya mifugo kwa ajili ya kulisha kiangazi, sasa hivi tunazalisha na mbegu za malisho bora ambayo wakulima wanatakiwa wayapande kwenye maeneo yao na hii itasaidia kukabiliana na migogoro ya ardhi," alisema Dk. Chang'a.

Alisisitiza kuwa kwa wafugaji ambao hawana uwezo wa kupanda malisho kwa ajili ya mifugo yao, wanatakiwa watumie mbinu ya kutunza mabaki ya mazao mbalimbali yakiwamo mahindi na maharage kwa ajili ya kulishia mifugo yao wakati wa kiangazi.

Dk. Chang'a alisema katika idara ya ufugaji wa ndege, taasisi hiyo inawashauri Watanzania wenye kipato cha chini kufuga zaidi kuku wa kienyeji ambao gharama zake ni ndogo kutokana na kuwa wavumilivu wa magonjwa na wanatumia chakula kidogo.


Aliwataja baadhi ya ndege ambao ufugaji wake ni rahisi kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuwa ni kuku, bata, kanga, kwale na bata mzinga.

Kuhusu sekta ya uvuvi, Dk. Chang'a alisema wananchi wanatakiwa kutumia mbegu bora za samaki ambao wamefanyiwa utafiti na wanastahimili mazingira ya aina mbalimbali ikiwamo maji ya baridi.

"Sasa hivi tunawashauri wafugaji wa samaki kufuga samaki kwenye mabwawa ambao biashara yao kwa sasa ni kubwa. Kuna baadhi ya mabwawa rahisi ambayo wataalamu wamebuni unaweza kutengeneza hata ndani ya nyumba yako," alisema Dk. Chang'a.

Hata hivyo, alisema ziko taasisi mbalimbali za serikali na za binafsi ambazo zinahamasisha ufugaji, hivyo akawataka wananchi kuzitembelea kwa ajili ya kujifunza na kununua mbegu bora za mifugo husika.

Maonyesho ya Nanenane Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanashirikisha mikoa saba ambayo inaongoza kwa uzalishaji wa chakula na kutokana na sifa hiyo imebatizwa jina la 'Big Seven (zamani ilikuwa Big Four kabla ya kugawanywa kwa mikoa ya Iringa, Mbeya na Rukwa).





# Shein: Serikali kazi yake kuwahudumia wananchi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, amesema kazi kubwa ya serikali inayoiongoza ni kuwahudumia wananchi kwa sababu wao ndio waliyoiweka madarakani.

Aliyasema hayo jana kisiwani Pemba wakati akizungumza na wananchi baada ya kuweka jiwe la msingi Ofisi za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (ZSSF), Ofisi za Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na kuzindua hoteli ya mkoani iliyofanyiwa ukarabati mkubwa.

Dk. Shein alisema kazi ya serikali ni kuwaletea maendeleo wananchi na kwa sasa Serikali ya Awamu ya Saba imefanya hivyo kwa vitendo ikiwa ni pamoja na kuwasogezea huduma muhimu za kimaisha.

Alisema kuzinduliwa kwa hoteli ya mkoani ambayo ni miongoni mwa hoteli za serikali zilizojengwa mwanzoni mwa miaka 1970 na ya Chakechake na Wete Pemba, ambazo zilikuwa chini ya Shirika la Utalii Zanzibar, ambalo kwa sasa halipo ilikuwa ni kuwahudumia wananchi wa ndani na nje ya nchi.

Alisema hoteli ni kwa ajili ya watu mbalimbali wakiwamo watalii na wananchi ambao wanapata huduma za kitalii, hatua hiyo inaimarisha utalii wa ndani. Alisema serikali zilizopita za kikoloni hazikuimarisha sekta ya kitalii na badala yake Serikali ya Zanzibar imeimarisha kwa kiasi kikubwa sekta hiyo na kuongezeka kwa hoteli na wageni.

Kwa upande wa hatua za serikali za kujenga jengo la ofisi za ZRB Pemba, Dk. Shein, alisema hatua hiyo itasaidia kukusanya kodi kwa ajili ya mapato ya Zanzibar.

"Tukisema wengine wanaguna na wagune mpaka wagunuke sisi tunasonga mbele kubwa ninalowaambia wananchi wa mkoani wajiandae kupokea wageni...Serikali imeridhika na mimi mwenyewe nimeridhika," alisema Dk. Shein.

Alisema ZRB imefanya kazi kubwa na ndio maana uchumi wa Zanzibar umeimarika na hivi sasa kufikia uchumi wa kati kama ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara na sasa uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia saba.

Alisema ZSSF imeanzisha miradi mbalimbali mikubwa Unguja na Pemba hatua ambayo imesababisha kukua na kuimarika kwa miji yote ya Zanzibar.

Naye Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohammed Ramia Abdiwawa, alisema mafanikio yaliyopatikana kutoka Mfuko wa ZSSF na kutoa historia ya ujenzi wa hoteli kisiwani humo.

"Niwatoe wasiwasi wananchi ambao ni wanachama wa Mfuko wa ZSSF pesa zao zipo salama," alisema Balozi Ramia.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Khamis Mussa, alisema hoteli ya Mkoani Pemba, ilifunguliwa Januari 9, mwaka 1974 na kutoa huduma kwa miaka 1970 hadi 1990, lakini kutokana na kukosa matunzo hoteli hiyo ilichakaa na kusitisha kutoa huduma zake.

Alisema chini ya uongozi wa Rais Dk. Shein, Baraza la Mapinduzi liliamua kuikabidhi hoteli hiyo kwa ZSSF kwa lengo la kuifufua na kuiendeleza kiuchumi kama lengo la awali na makabidhiano rasmi yalifanyika Oktoba 19, mwaka 2018.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akiwahutubia wananchi, wakati wa hafla ya ufunguzi wa hoteli ya Mkoani Pemba juzi iliyokarabatiwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF). **PICHA: IKULU**

# TAMWA yawapa somo wanawake waliotelekezwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi za Zanzibar, kimewataka baadhi ya kinamama waliotelekezwa na waume zao kutokata tamaa, badala yake wajikite katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ili wajikwamue kimaisha.

Ofisa Masoko, Muhidini Ramadhan, alisema hayo wakati alipokua akizungumza na kinamama hao ofisi za chama hicho, Tunguu Wilaya ya Kati Unguja, katika hafla maalumu ya kuwakabidhi vifaa ambavyo vitatumika kwa ajili ya uzalishaji wa sabuni.

Aliwataka kutumia vyema fursa hiyo ya kupatiwa vifaa ili waweze kuzalisha sabuni ambazo zitawaingizia kipato na kujikimu.

Alisema kwa muda mrefu baadhi ya kinamama kwenye familia wamekuwa wakikumbwa na hali ya utelekezwaji na kusababisha kuhangaika wao na watoto.

Meneja miradi wa chama hicho, Asha Abdi Makame, aliwataka kutumia vyema nyenzo hizo ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Alisema ni wajibu wao kuhakikisha wanazalisha bidhaa bora ambazo zitauzika sokoni na kupendwa na wengi.

"Nendeni mkatumie vifaa hivi kwa uangalifu mkubwa na msiwe tayari kutumia kwa matumizi mengine yasiokusudiwa," alisema.

Baadhi ya wanaufaika wa msaada huo walisema umekuja wakati muafaka na wanahitaji kuungwa mkono ili kupata fedha za kujikimu

# Wananchi kutafuta ufumbuzi dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

VIONGOZI wa Ushirika wa Kilimani Zanzibar, wameahidi kushirikiana na wananchi kutafutia ufumbuzi matatizo yanayowakabili ikiwamo utumiaji wa dawa za kulevya kwa vijana.

Katibu wa Ushirika huo, Kombo Juma Maalim, alisema hayo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusiana na ushirika huo.

Alisema tangu kuanzishwa kwa ushirika huo, wamesaidia kupunguza wimbi la vijana kutumia dawa za kulevya.

Alisema wamewakusanya vijana hao na kuwapa elimu ya ujasiriamali ili kuanzisha miradi kwa lengo la kupata fedha za kujikimu kimaisha na kuachana na matumizi ya dawa hizo.

Alisema vijana hao wamewapeleka katika nyumba za kurekebisha tabia (sober house) ili waachane na matumizi ya dawa hizo.

Aliwaomba wananchi kuunga mkono ushirika huo ili kufanya kazi kwa bidii na kufikia malengo yaliokusudiwa ili kuisaidia jamii.

Aliwataka wananchi na familia za vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya kuwa nao pamoja vijana hao katika harakati mbalimbali za kimaendeleo.

"Zipo baadhi ya familia zinawatenga vijana walioacha matumizi ya dawa za kulevya, hivyo si jambo jema kuwatenga na badala yake kuwa nao pamoja," alisema.

# MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA VYETI



**Nelius France Binomtonzi** amepotelewa na vyeti vyake, cha kidato cha nne chenye index Na. **S088-0082** cha Kaigara Sekondari kilichotolewa 2006, cheti cha chuo cha utafiti na kilimo (MATI MARUKU) cha 2010 na cheti cha matokeo (transcript) cha MATI MARUKU cha mwaka 2010.
Alipotelewa na begi lake lililokuwa na vyeti hivyo. Ametoa taarifa polisi na kupewa Na. **MOR/MOR/RB/446370/2019,** kwa yeyote atakayeviona atoe taarifa polisi au awasiliane naye kwa Na. **0768-037949 au 0763-310772.**

115848202

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## HATI YA KIAPO

Mimi **BENUARD ALEX MAPUNDA** wa S.L.P 1396-Tanga, mtu mzima mwenye akili timamu, naapa na kuthibitisha mbele ya Hakimu/Wakili Mahakamani kama ifuatavyo:-

1. Kwamba, mimi **BENUARD ALEX MAPUNDA** ni mmiliki wa gari yenye namba za usajili T 401 DEF Toyota Brevis.
2. Kwamba, kadi ya gari hiyo imepotea na nimeitafuta bila matumaini ya kuipata tena.
3. Kwamba,kwa kiapo hiki naiomba mamlaka husika inipatie kadi nyingine ya gari hiyo **T 401 DEF** Toyota Brevis kwa jina la **BENUARD ALEX MAPUNDA.**

**UTHIBITISHO**
Mimi **BENUARD ALEX MAPUNDA,** nathibitisha kuwa yote niliyoyasema hapo juu kuanzia aya ya 1-3 ni kweli tupu kwa jinsi nijuavyo na kwa mujibu wa sharia ya viapo (The Oaths and Statutory Declaration Act.Cap.34 R.E.2002)

Imethibitishwa hapa Tanga
Leo tarehe 04/8/2020
Mbele ya ...
Cheo ...
Anuani ...
Sahihi ...
Sahihi ya muapaji
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

115847602

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA

MAOMBI MADOGO NA. 97/2020

BIBIANA CLEMENCE MULONGO ....................................MDAI

DHIDI YA

1. FRED MUSHUMBUSI RWEGASIRA
2. VEDASTO KAPARANGABO............................WADAIWA

KWA:- FRED MUSHUMBUSI RWEGASIRA (POPOTE PALE MLIPO)

Mnaarifiwa/ unaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na. 97/2020 yamepangwa kutajwa tarehe 15/09/2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/ mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 05/08/2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

115848002

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;208/2020

Ombi la ALLAN KENNETH MUHANDO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ASSA RAMA MUHANDO.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 04/08/2020.

115848102

---

## KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA

**ABDI MAGOGO KIHIYO WA P.O.BOX 584 KOROGWE**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA (PLOT NO 16 BLOCK `A' KILICHOPO BAGAMOYO .
SURVERY REG PLAN NO **73167** MEARING **1648 M2**
YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI
**TAARIFA ZA POLISI: KOR/RB/3306/2020**

115846802

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKSON KENETH MSALILWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0639-0122** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2006 katika shule ya Sekondari Udzungwa. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **IRI/MUF/RB/576214/2020**

215846902

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI

(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;212/2020

Ombi la SIFA MAKALA,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MAKALA MASIMBA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 12/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/08/2020.

Tarehe 5/8/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115847302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI

(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;214/2020

Ombi la BONIFACE RAPHAEL NDAHELEWE,-Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JOHN RAPHAEL NDAHELEWE.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/08/2020.

Tarehe 05/8/2020
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

215847402

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MOROGORO.

SHAURI LA MADAI NA.22 YA 2018

MARGARETH SARAMAKI STEPHEN........MSHINDI TUZO

DHIDI YA

BENROSE TANZANIA LIMITED...........MSHINDWA TUZO

## WITO WA MAHAKAMA

KWA: BENROSE TANZANIA LIMITED

Wito huu ni wa kesi tajwa hapo juu,ambayo imepangwa kutajwa kwa utekelezaji tarehe 27 mwezi wa 8 mwaka 2020 saa2:30 asubuhi mbele ya mahakama ya hakimu mkazi Morogoro.

Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote aliyeidhinishwa kusimama kwa niaba yako na pia unatakiwa kutoa maelezo yako siku hiyo nakala zote za ushahidi utakazotumia kwanini utekelezaji usiendelee dhidi yako.

Zingatia kwamba,Kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu,Mahakama itaendelea na kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.

Imetolewa chini ya Muhuri wa Mahakama leo siku ya Tarehe 24 mwezi 7 mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI
MOROGORO
RESIDENT MAGISTRATE I/C
MOROGORO

215847502

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI

( S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2

Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO

Usimamizi wa mirathi No;209/2020

Ombi la VERONICA DONALD MTETEMELA,-Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ROMANUS MWEZIMPYA LUOGA.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 14/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 05/08/2020.

215847202

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**Mohamed Salehe** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0156-0015** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2000 katika shule ya Sekondari Tanga. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **UD/RB/615/2009**

115846702


**OFISI ZA MATANGAZO**
Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam.
Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
website: www.ippmedia.com



Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waliofariki kwa mlipuko Lebanon zaidi ya 100

**BEIRUT, Lebanon**

WAFANYAKAZI wa uokozi wanaendelea kuwatafuta watu waliofukiwa kwenye vifusi vya majengo yaliyoporomoka, siku moja baada ya mlipuko mkubwa kutokea katika bandari ya Beirut na kuwaua karibu watu 100.

Mkuu wa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini humo, George Ketteneh, alieleza kuwa karibu watu 4,000 wamejeruhiwa na huenda idadi ya vifo ikaongezeka.

Ofisa mmoja wa ulinzi wa kiraia alisema bado wanawatafuta karibu watu 100 waliofukiwa kwenye vifusi, hasa karibu na Bandari ya Beirut.

Raia wa Lebanon juzi waliamka na kushuhudia uharibifu mkubwa uliotokea katika bandari hiyo pamoja na maeneo ya karibu katikati mwa mji huo mkuu.

Wafanyakazi wanaendelea kuondoa vifusi ili kufungua barabara na kukarabati maeneo yaliyoharibiwa.

Baraza la Mawaziri la Lebanon lilifanya kikao cha dharura jana baada ya Baraza Kuu la Ulinzi la nchi hiyo, kuitangaza Beirut kuwa eneo la janga na kupendekeza hali ya hatari kwa wiki mbili.

Mapema jana, vikosi vya uokozi vilikuwa vikiondoa mabaki ya vitu ili kufungua barabara pamoja na kuanza matengenezo baada ya kutokea kwa mlipuko huo na kuharibu sehemu kubwa ya majengo, magari na kuzusha taharuki kwa wakazi wa mji wa Beirut.

Hadi sasa ripoti zinasema chanzo cha mlipuko huo ni moto uliozuka katika ghala moja iliyohifadhi shehena na kemikali hatari ya Amonium Nitrate ambayo ilikamatwa karibu miaka sita iliyopita.

Katika hotuba yake kwa Taifa, Waziri Mkuu wa Lebanon, Hassan Diab, alitoa wito kwa mataifa yote na marafiki wa nchi yake kutoa msaada kwa Taifa hilo dogo, akisema linashuhudia janga kubwa kutokana na maafa ya mkasa wa mjini Beirut.

Diab pia ameahidi kuchukua hatua kwa wote waliohusika na kutokea kwa janga hilo.

"Kilichotokea hakitopita bila uwajibikaji, wale wanaohusika watalipa kutokana na janga hili. Hii ni ahadi kwa waliopoteza maisha na waliojeruhiwa. Hii ni azma ya Taifa, kutakuwa na ukweli uliotangazwa kuhusu ghala hatari ambalo limekuwapo tangu mwaka 2014, kwa miaka sita," amesisitiza Diab.

Tangu kutokea kwa tukio hilo, mataifa mbalimbali duniani yameendelea kutuma salamu za pole na rambarambi kwa Lebanon, huku mengi yakiahidi kutuma msaada wa uokozi na fedha kuisaidia nchi hiyo kupambana na maafa yaliyotokea.

Nchi za Iran, Ufaransa, Ubelgiji, Jamhuri ya Czech, Uturuki na Uholanzi na Uingereza ni miongoni mwa mataifa yaliyosema yanatuma waokoaji na shehena za vifaa na vyakula kwenda mjini Beirut kuongeza juhudi za utafutaji wahanga na kuwasaidia waliojeruhiwa.

Israel pia ambayo imekuwa kwenye mvutano na Lebanon imesema iko tayari kuwatibu majeruhi wa mlipuko wa mjini Beirut.

Mlipuko huo ambao ni mbaya katika historia ya Taifa hilo la Mashariki ya Kati umetokea wakati Lebanon inakabiliwa na mzozo mkubwa wa kiuchumi kuwahi kushuhudiwa tangu kumalizika kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya mwaka 1975-1990.

Tayari Rais wa Lebanon, Michel Aoun, ametangaza kuwa serikali itatoa dola milioni 66 kusaidia kupunguza athari za tukio hilo kwa taifa hilo ambalo mbali ya mzozo wa uchumi linazongwa pia na kadhia ya janga la virusi vya corona.

*DW*



Wafuasi wa Chama cha FCC Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) wakiwa katika maandamano mjini Bukavu, kuunga mkono kumtaka Rais wa nchi hiyo, Félix Tshisekedi, kuheshimu katiba. **PICHA: REUTERS**

## UN yafunga kambi mbili za wakimbizi Mali, Niger

**BAMAKO, Mali**

UMOJA wa Mataifa (UN), umezifunga kambi mbili za wakimbizi katika nchi za Mali na Niger.

Takribani raia 15,000 wa Mali wamehamishwa kutoka kambi mbili kubwa za wakimbizi Magharibi mwa Niger, mwishoni mwa mwaka wa 2019 ili kuishi katika miji ya karibu na salama kutokana na mashambulizi ya makundi ya itikadi kali.

UN imesema kufungwa kwa kambi hizo Desemba 2019 ulikuwa uamuzi wa pamoja wa Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) na serikali ya Niger na likaharakishwa mwaka jana kufuatia kuzorota kwa hali ya usalama.

Kambi hizo katika maeneo ya Tabarey Barey na Mangaize ziliwahifadhi raia wa Mali wanaokimbia machafuko katika nchi yao tangu mwaka wa 2012.

Eneo la Magharibi mwa Niger hushuhudia mashambulizi ya mara kwa mara ya makundi ya itikadi kali.

Mashambulizi katika kambi za Tabarey Barey na Mangaize yaliwaua wakimbizi 10 na maofisa wa Jeshi la Niger waliokuwa wakitoa ulinzi kati ya mwaka 2014 na 2016.

**DW**

**UN imesema kufungwa kwa kambi hizo Desemba 2019 ulikuwa uamuzi wa pamoja wa Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) na serikali ya Niger na likaharakishwa mwaka jana kufuatia kuzorota kwa hali ya usalama.**

# Mazungumzo bwawa la Ethiopia kizungumkuti

**CAIRO, Misri**

MISRI imeamua kujiondoa kwenye mazungumzo kati yake na Ethiopia kuhusu bwawa kubwa la kuzalisha umeme ambalo ujenzi wake umegharimu mabilioni ya dola kwenye Mto Blue Nile.

Misri imesema itafanya majadiliano ya ndani baada ya Ethiopia kutoa mapendekezo mapya, kuhusu namna ya kujaza bwawa hilo lililoibua utata.

Wizara ya Umwagiliaji Sudan imesema kwamba msimamo wa sasa wa Ethiopia umesababisha hofu namna mazungumzo hayo yanavyostahili kuendeshwa.

"Tunasisitiza kuhusu hatari iliyopo kutokana na ujenzi wa bwawa hilo na watu wa Sudan, ikiwamo hatari kwa mazingira na kwa jamii, pamoja na usalama wa mamilioni ya watu wanaoishi kando mwa Mto Nile," ilieleza taarifa ya Wizara ya Umwagiliaji ya Sudan.

Bwawa hilo la Grande Renaissance, ambalo limejengwa kilomita 15 kutoka mpaka wa Ethiopia na Sudan, limesababisha mgogoro kati ya nchi hizo tatu.

Misri ina hofu kwamba mradi huo wa dola bilioni nne unaweza kusababisha hali ya kupungua kwa maji kwa ajili ya kilimo na matumizi ya kawaida nchini Misri, huku Sudan ikiwa na hofu kuhusu usalama wa watu wake, kutokana na bwawa hilo.

Misri inategemea Mto Nile kwa asilimia 90 ya maji kwa ajili ya matumizi ya shughuli zake.

Misri imeeleza kuwa Ethiopia imewasilisha mapendekezo ya kuendesha bwawa hilo bila kuwapo mpango maalum wa kisheria wa namna ya kusuluhisha migogoro.

Waziri wa Umwagiliaji wa Ethiopia, Seleshi Bekele, alikuwa ameeleza matumaini ya kupatikana mafanikio kwenye mazungumzo hayo na alikuwa ameandika ujumbe kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter akisema: "Ethiopia ingependa kusaini mkataba wa kujaza bwawa hilo haraka iwezekanavyo na kuendelea na mazungumzo ili kukamilisha mkataba mpana".

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, alisema kwamba nchi yake imeshajaza nusu ya bwawa hilo kutokana na mvua kubwa.

*VOA*



# LUKAKU

## ATAKA INTER KUIMARIKA EUROPA

**MILAN, Italia**

ROMELU Lukaku tayari anaangalia mbele baada ya kuisaidia Inter Milan kutinga robo fainali ya Ligi ya Europa, Jumatano.

Mabao kutoka kwa Lukaku na Christian Eriksen yalishuhudia Inter ikiichapa Getafe mabao 2-0 mjini Gelsenkirchen na kutinga hatua hiyo.

Lukaku amefikisha mabao 30 msimu huu kwa mara ya kwanza katika maisha yake ya soka na alikosa nafasi nzuri zaidi kipindi cha pili.

Straika haraka alisahau kuhusu kupoteza nafasi ya kuongeza bao kwenye mchezo huo.

"Kukosa? Mambo haya yanatokea kwenye soka, lakini kila kitu ni kufikiria mchezo ujao," alisema Lukaku akiiambia Sky Sport.

"Nataka kushinda na kuendelea kuisaidia timu. Kazi tunayofanya na kocha kwa hakika ni nzuri na muhimu sana kwetu.

"Timu inakua na tunahitaji kusonga mbele na morali hii na ari ya kuimarika zaidi."

Jorge Molina alikosa penalti dakika ya 76 kwa Getafe wakati Inter sasa ikiisubiri kati ya Rangers au Bayer Leverkusen kwenye robo fainali.

# DORTMUND YAIKANA UNITED DILI LA SANCHO

**DORTMUND, Ujerumani**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Borussia Dortmund, Hans-Joachim Watzke amesisitiza hakuwa na "mawasiliano" na Manchester United kuhusu Jadon Sancho.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa sana na miamba hao wa Ligi Kuu ya England, huku taarifa za hivi karibuni zikibainisha kwamba dili hilo lenye thamani ya pauni milioni 108.5 lilikuwa limekaribia kukamilika.

Hata hivyo, Watzke amekanusha ripoti hizo, akisema hakuna mawasiliano yoyote kati ya klabu hizo kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

"Hadi sasa, hakujawa na mawasiliano kati ya Borussia Dortmund na Manchester United katika suala la Sancho," alisema akiiambia Suddeutsche Zeitung, Jumatano.

United imeripotiwa kwamba inajiandaa kuachana na dili hilo la Sancho kwa sababu hawapo tayari kulipa bei inayotakiwa na Dortmund.

Mkurugenzi wa soka wa Dortmund, Michael Zorc alisema anatarajia Sancho kuwa kwenye klabu hiyo msimu wa 2020-21.

"Nina uhakika kwamba, Jadon atakwenda kwenye mazoezi Jumatatu na atakuwa na sisi kwa misimu inayokuja," alisema akiiambia Suddeutsche Zeitung.




# BALE ATEMWA REAL IKIIVAA MAN CITY

**MADRID, Hispania**

GARETH Bale ameachwa katika kikosi cha Real Madrid kwa ajili ya mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City, utakaopigwa leo Ijumaa.

Nyota huyo wa kimataifa wa Wales hakutajwa katika kikosi cha wachezaji 24 waliosafiri na timu, lakini nahodha, Sergio Ramos, ambaye amefungiwa kucheza mchezo huo wa pili wa hatua ya 16, amejumlishwa.

James Rodriguez pia ameachwa, pamoja na straika Mariano Diaz, ambaye alipimwa na kukutwa na virusi vya corona wiki iliyopita na amejitenga.

Eden Hazard yupo kikosini licha ya mashaka juu ya ufiti wake baada ya kuumia kifundo cha mguu, huku Luka Jovic, ambaye alianza kwenye mchezo mmoja wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa Madrid, pia akijumuishwa.

Madrid wapo nyuma kwa mabao 2-1 waliyofungwa kwenye mchezo wa kwanza pale katika dimba la Santiago Bernabeu.

Bale amekuwa hana mahusiano mazuri na kocha mkuu, Zinedine Zidane na nyota huyo wa zamani wa Tottenham amecheza mara mbili tu tangu kurudi kwa msimu wa Ligi ya Hispania, Juni, mwaka huu.

Mchezaji mwenzake, Casemiro alisisitiza kwamba, Bale bado ana sapoti ya makocha wa Madrid na wachezaji licha ya hali anayoipitia hivi sasa na kwamba "sio bora kwa kipaji chake."




# GUNDOGAN: HAVERTZ NI BORA KULIKO BALLACK

**LONDON, England**

NYOTA anayeripotiwa kuwaniwa na Chelsea, Kai Havertz ni bora zaidi ya kiungo wao wa zamani, Michael Ballack, kwa mujibu wa Ilkay Gundogan.

Bayer Leverkusen inataka angalau euro milioni 78 ili kumuachia Havertz, ambaye amefunga mabao 29 na kutoa pasi za mwisho tisa kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, tangu kuanza kwa msimu wa 2018-19.

Nyota wa Manchester City, Gundogan anamtambua nyota mwenzake huyo wa Ujerumani kuwa ni mchezaji tofauti na Ballack, ambaye alikuwa mshindi wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Leverkusen na Chelsea, pamoja na fainali ya Kombe la Dunia na Ujerumani.

Havertz amecheza kwa kiwango cha kuvutia zaidi kwa misimu miwili iliyopita na Gundogan ni shabiki mkubwa kwa staili yake kuliko ile ya Ballack.

"Natarajia mambo makubwa kutoka kwake. Kai ni mchezaji asiyezuilika," amesema Gundogan akiliambia gazeti la Sport Bild.

"Ana mambo mengi uwanjani na anakipaji kinachomtambulisha kwa haraka. Ni mchezaji ambaye utafurahia kucheza naye.

"Kwa maoni yangu, Havertz ni bora zaidi ya Ballack katika suala la mchezaji bora na mwenye mbinu."



# JESUS: TUMEMWANGUSHA DE BRUYNE MSIMU HUU

**MANCHESTER, England**

GABRIEL Jesus anahisi Manchester City wamemuangusha mfalme wao wa pasi za mwisho, Kevin De Bruyne msimu huu.

Jesus na De Bruyne ndio walikuwa waamuzi wa mchezo kipindi cha pili wakati City ikiifunga Real Madrid mabao 2-1 pale kwenye dimba la Santiago Bernabeu, Februari.

Mchezo wa pili uliosubiriwa kwa muda mrefu wa hatua ya 16 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, utapigwa leo Ijumaa katika dimba la Etihad.

De Bruyne amekuwa na msimu wa kuvutia baada ya kufikia rekodi ya Thierry Henry ya kuwa na pasi za mwisho 20 kwenye msimu mmoja wa Ligi Kuu ya England.

Bado, mshambuliaji wa Brazil, Jesus anahisi idadi hiyo ingeweza kuongezeka, akisisitiza City muda mwingi walikuwa wanapoteza mpira langoni licha ya kufunga mabao 102 kwenye Ligi.

"Nafikiri katika kila mchezo anaweza kutengeneza pasi za mwisho tatu au nne kwa upande wetu," alisema akiiambia tovuti ya klabu hiyo.

"Msimu huu tumekosa mabao mengi, kama si, Kevin angeweza kufikisha pasi za mwisho 30. Yeye ni mchezaji mzuri.

"Na mara zote amekuwa akiwaangalia washambuliaji. Ni jambo zuri sana kucheza naye."




# SANCHEZ SASA JUMLA INTER

**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer amethibitisha Alexis Sanchez atajiunga na Inter Milan kwa mkataba wa kudumu.

Ofisa Mtendaji wa Inter, Giuseppe Marotta, alisema Jumatano kwamba anatarajia kutangaza usajili wa Sanchez, ambaye amekuwa akicheza kwa mkopo hapo San Siro msimu huu, kwa mkataba wa miaka mitatu, jana Alhamisi.

Akizungumza baada ya United kushinda mabao 2-1 dhidi ya LASK kwenye mchezo wa pili wa hatua ya 16-bora ya Ligi ya Europa, Solskjaer alimtakia Sanchez kila la heri nchini Italia, ambako ameanza kurudi kwenye kiwango chake baada ya kuwa na wakati mgumu pale Old Trafford.

"Naweza kuthibitisha kwamba amekubali na sisi tumekubali," alisema Solskjaer. "Alexis amefurahia muda wake kule.

"Walimpenda yeye, bila shaka huo ni wakati mzuri kwake. Tunamtakia kila lililo bora. Yeye ni mchezaji mkubwa ambaye anataka kuona ubora wake kwenye soka.

"Kwa sababu yoyote, hatukuona ubora wa Alexis, lakini ni mchezaji wa daraja la juu na tunamtakia kila la heri."

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA YATANGAZA SIKU YA MESSI KUSTAAFU SOKA

●●●Ni baada ya mitatu au minne ijayo, amesema anataka kumaliza kipindi chake cha kucheza akiwa...

**BARCELONA, Hispania**

LIONEL Messi atastaafu kama mchezaji wa Barcelona ndani ya miaka "mitatu au minne ijayo", kwa mujibu wa Rais wa Klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu.

Mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, Messi mkataba wake wa sasa pale Camp Nou unamalizika mwishoni mwa msimu 2020-21, lakini Bartomeu mwezi uliopita alisema anatarajia nyota huyo atasaini kuongeza mwingine.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, amekuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake ya utotoni ya Newell's Old Boys ya nchini Argentina kabla ya kutundika daluga.

Hata hivyo, Bartomeu hana shaka kwamba mfungaji huyo wa wakati wote wa Barca, Messi atamalizia kipindi chake cha uchezaji kwa miamba hao wa Catalunya, jambo ambalo linaweza kutokea mwaka 2023.

"Si mimi tu ninayesema hivyo. Messi anasema yeye mwenyewe, kwamba anataka kumaliza kipindi chake cha kucheza soka hapa Barcelona na ndio klabu pekee kwake," alisema Bartomeu akiiambia beIN SPORTS.

"Sina shaka yoyote kuhusu hilo kwamba wakati atakapomaliza kipindi chake cha kucheza ndani ya miaka mitatu au minne ijayo, itakuwa hapa Barcelona. "Messi yupo wazi kabisa. Amekuwa hapa tangu akiwa mtoto. Anajua rangi yake na yeye ni sehemu ya historia ya klabu hii.

"Yeye ni mchezaji bora duniani. Si tu sasa, lakini katika historia ya mchezo wenyewe. Yupo hapa Barcelona na ameweka wazi kwamba anataka kubakia hapa."

Jambo jingine muhimu kwa Bartomeu ni kujaribu kumbakiza golikipa, Marc-Andre ter Stegen asaini mkataba mpya, kwani ule wa sasa umebaki miaka miwili tu kumalizika.

"Marc ni mchezaji mwenye akili na mtu bora, na ameonyesha hayo yote akiwa golikipa wetu," alisema Bartomeu.

"Kutokana na hali hii ya mlipuko wa COVID-19, alisema, 'ngoja tusubiri jambo kwa utulivu kuzungumzia kuhusu majaliwa ya baadaye.' Lakini majaliwa yake ni kuongeza mkataba na Barca."

## KWA UFUPI

**COUNTIHO AKARIBIA ARSENAL**

MCHAKATO wa winga wa Barcelona, Philippe Coutinho mwenye umri wa miaka 28, kuhamia Arsenal unaelekea kukamilika. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil msimu uliopita alikuwa Bayern Munich kwa mkopo. ***(Sport)***

**MAN CITY KUSAJILI WANNE**

MANCHESTER City wanataka kusajili wachezaji wanne zaidi kipindi hiki cha majira ya joto. Mlinzi wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 29 raia wa Senegal na straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez mwenye miaka 22 raia wa Argentina ni miongoni mwa wanaowaniwa. ***(Sky Sports)***

**WILLIAN KIMEELEWEKA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal imempa mkataba wa miaka mitatu winga wa Chelsea na Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 31. ***(Sky Sports)***

**CHELSEA, GIMENEZ PAZURI**

CHELSEA ina nafasi nzuri zaidi ya kumsajili mlizni wa Uruguay ambaye thamani yake ni pauni milioni 60, Jose Gimenez mwenye umri miaka 25, kutoka Atletico Madrid baada ya kushinda kumchukua kiungo wa West Ham na England, Declan Rice. ***(Daily Star)***

**SERGION NJIA NYEUPE CHELSEA**

KLABU ya Chelsea ipo katika hatua nzuri kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa kushoto wa Real Madrid, Sergio Reguilon mwenye umri wa miaka 23, ambaye alitumia msimu uliopita akicheza kwa mkopo kule Sevilla. ***(ESPN)***

**STERGEN KUSAINI MI5 BARCA**

GOLIKIPA wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen anatarajia kusaini mkataba mpya wa miaka mitano na klabu hiyo ya Hispania. Na hilo litaikata maini Chelsea, ambao walikuwa wanamfuatilia kwa karibu kipa huyo wa kimataifa wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28. ***(Mundo Deportivo via Sun)***

**ARSENAL KASI KWA GABRIEL**

ARSENAL inaongoza kwenye mbio za kumsajili mlinzi wa Lille na Brazil, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, mbele ya Manchester United, Everton na Napoli. ***(La Voix du Nord via Daily Star)***

**RODRIGUEZ HUYO ATLETICO**

KIUNGO wa Real Madrid na Colombia, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 29, anatarajiwa kukamilisha usajili wa pauni milioni 13.5 kwenda kwa wapinzani wao wa jiji moja, timu ya Atletico Madrid. ***(El Golazo de Gol via Sun)***

**SPURS KUMUUZA AURIER**

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kumuuza mlinzi wake wa pembeni mwenye thamani ya pauni milioni 35, Serge Aurier, huku AC Milan na Monaco zote zikimwania nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 27. ***(Mirror)***

**BREMEN YAMTAKA CHONG**

WERDER Bremen wanataka kumchukua kwa mkopo nyota wa Manchester United, Tahith Chong mwenye umri wa miaka 20 raia wa Uholanzi. ***(Bild)***

**PALACE YAMUWANIA FRASER**

KLABU ya Crystal Palace imetoa ofa ya mkataba kwa winga wa Scotland, Ryan Fraser. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kuondoka Bournemouth. ***(Guardian)***

## HABARI MICHEZO

**JEZI...**




Meneja Bidhaa na Huduma za Kibenki kutoka Benki ya NBC, Jonathan Bitababaje (kulia), akikabidhi jezi za mpira wa miguu kwa nahodha wa timu ya RAS Mara, Jedi Kuyenga, ikiwa ni sehemu ya udhamini wa benki hiyo kwenye Bonanza la Michezo lililofanyika jana, kwenye viwanja vya Maonyesho ya Kilimo ya Nanenane yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MBEYA CITY YATAMBA KUSAJILI SIMBA, YANGA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City imetamba kuwa itasajili mchezaji yoyote yule mzawa kutoka klabu za Simba na Yanga, lakini inaweza kuwanyang'anya wachezaji inayowahitaji kutokana na fungu la maana la usajili walilonalo kwa sasa.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Oscar Kapinga alisema jana kuwa baada ya kutofanya vema msimu uliomalizika kiasi cha kusubiri dakika za mwisho, kwa sasa wameona waanze mapema kuitengeneza timu yao kwa msimu ujao, na tayari wana fungu la pesa za usajili.

"Tumejifunza kutokana na makosa, hatutosubiri tena aibu hii iliyotufika msimu uliomalizika wa kusubiri dakika za mwisho na mechi za mwisho za Ligi Kuu ndiyo tubaki, ndiyo maana tumejiandaa mapema, tayari tuna fungu la kutosha, tunasubiri tu ripoti ya mwalimu atuambie ni eneo gani lina mapungufu na mchezaji gani anamhitaji," alisema Kapinga.

Aliongeza kuwa kwa pesa walizonazo wana uwezo kabisa kusajili wachezaji wanaotoka Simba au Yanga, lakini wale ambao wanawaniwa na timu hizo.

'We subiri tu uone, utakuwa usajili wa kufuru, hatutaki tena mzaha, mchezaji kutoka Simba au Yanga sisi tunaweza kumsajili na hata anayewaniwa na timu hizo, tunaweza kutia mguu kumsajili, Mbeya City ya msimu ujao itakuwa moto," alisema mwenyekiti huyo.

Akieleza sababu ya kutofanya vema msimu huu, mwenyekiti huyo alisema timu ilikuwa na wachezaji wengi chipukizi wasio na uzoefu wa ligi, lakini kubadili makocha mara kwa mara, na pia ikasajili wachezaji wengi wa dirisha dogo.

"Mimi niliingia madarakani bado mechi 10, timu ilikuwa na changamoto, lakini tunashukuru tumebaki, kikubwa hatutorudia tena hali hii," alisema.

Mbeya City ilinusurika kwenye mechi ya mchujo dhidi ya Geita Gold, baada ya kutoka sare ya bao 1-1 ugenini na kabla ya kushinda 1-0 nyumbani, hivyo kubaki Ligi Kuu.

**KITITA...**




Mshindi wa Bonasi ya Jackpot wiki iliyopita, Damiano John, akikabidhiwa mfano wa hundi ya shilingi 13,425,330 na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. **PICHA: SPORTPESA**

## Simba Queens kukabidhiwa Kombe lao Mwanza

**Na Saada Akida**

SHIRIKISHO la Soka Tanzania 'TFF' limeipongeza Simba Queens kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Wanawake msimu huu huku likieleza Agosti 12, mwaka huu wanataikabidhi rasmi kombe hilo baada ya mchezo wao wa mwisho dhidi ya TSC Queens ya jijini Mwanza.

Taarifa kutoka kwa Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, jana ilieleza kuwa sherehe za kukabidhiwa kombe hilo zitafanyia baada ya kumalizika kwa mchezo namba 132 dhidi ya TSC Queens katika Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

"Tunawapongeza Simba Queens kwa kutwaa ubingwa, pia sherehe za ubingwa zitafanyika Mwanza kwa kuwakabidhi kombe baada ya kumalizika kwa mechi yao dhidi ya TSC," alisema Ndimbo. Simba Queens juzi iliibuka na ushindi wa mabao 5 -0 mbele ya Baobab Queens kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake uliochezwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Matokeo hayo yanaifanya Simba Queens kufikisha pointi 53 baada ya michezo 20 wakati timu inayoifuata katika nafasi ya pili ni JKT Queens yenye alama 46 ikifutiwa na Ruvuma Queens pointi 44 huku timu zote zikiwa zimebakiza mechi mbili.

Mabao ya Simba yalifungwa na Mwanahamisi Omary aliyetupia mawili, Opah Clement alitupia bao moja, sawa na Dotto Evarist huku kipa Zubeda Mgunda akifunga moja kwa mkwaju wa penalti.

Simba imebakiza mechi za Kanda ya Ziwa pale jijini Mwanza dhidi ya Alliance Girls na TSC Queens ambayo itakuwa ya funga msimu.

Akizungumzia mafanikio hayo, nahodha wa Simba Queens, Mwanahamis Omari, alisema hawataki kuharibu ubingwa wao na wanahitaji kufanya vizuri katika mechi mbili zilizobaki kwa kupata matokeo mazuri.


Alisema tangu wamepoteza mechi moja kati ya 20, sasa hawataki kuona wanautia doa ubingwa wao kwa kupoteza mechi hizo mbili.

"Kila mechi kwetu ni fainali, hivyo hatutakuwa tayari kupoteza na kutia doa ubingwa wetu, tunaenda kupambana kutafufa matokeo ya mechi hizo za ugenini kwa kuvuna alama sita," alisema.

# Michezo

Ijumaa Agosti 7, 2020

Nipashe



Barca yatangaza siku ya Messi kustaafu soka

HABARI UK 22

UTANIUA BURE!...



Mshambuliaji wa LASK Linz, Marko Raguz, akimparamia mgongoni beki wa kati wa Manchester United, Harry Maguire, wakati akipambana kumdhibiti kwenye mechi ya Ligi ya Europa iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford na United kushinda 2-1. Hivyo kutinga robo fainali kwa tofauti ya mabao 7-1 kutokana na mechi ya awali ugenini kushinda 5-0. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAFUMUA NA KUSUKA

●●● Ninja akamilisha 'Ukuta wa Berlin', Yondani ndiyo hivyo tena, Juma Abdul aiambia nilipeni nisepe...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kufumua kikosi chake kwa kutimua wachezaji 14 na kubakisha 15 tu huku mabeki wake visiki, Kelvin Yondani na Juma Abdul mlango wa kutokea ukiwa wazi kwao, Klabu ya Yanga imeendelea kujiimarisha kwa kusuka safu ya ulinzi, imefahamika.

Ikionyesha dhamira yake ya kusuka safu imara ya ulinzi mithili ya 'Ukuta wa Berlin', jana Yanga ilikamilisha usajili wa beki wa kati, Abdallah Haji Shaibu 'Ninja', ambaye alisaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia, ikiwa ni mara yake ya pili kurejea kuichezea klabu hiyo.

Ninja aliitumikia Yanga katika msimu wa 2017/18 kabla ya kujiunga na MFK Vyskov ya Jamhuri ya Czech iliyomtoa kwa mkopo katika Klabu ya LA Galaxy ya Marekani.

Hata hivyo, alicheza kwa muda mfupi kabla ya kurejea katika Klabu yake ya MFK Vyskov ambako alikosa nafasi ya kudumu kwenye kikosi cha kwanza jambo lililomfanya kurejea nyumbani Tanzania na jana kusajiliwa tena Yanga.

Ninja ambaye anakuwa usajili wa tano kwa Yanga msimu huu, sasa ataungana na mabeki waliosajiliwa msimu huu, Bakari Mwamnyeto akitokea Coastal Union na Yasin Mustapha kutoka Polisi Tanzania kuunda safu imara ya ulinzi sambamba na Lamine Moro na Said Makapu waliobakisha kutoka kikosi cha msimu uliopita.

Wachezaji wengine waliosajili na Yanga dirisha hili linalotarajiwa kufungwa mwishoni mwa mwezi huu ni pamoja na kiungo Zawadi Mauya kutoka Kagera Sugar na mshambuliaji Wazir Junior kutoka Mbao FC.

Wakati huo huo, mabeki visiki wa Yanga, beki wa kati, Yondani na mlinzi wa pembeni, Abdul ambao ilielezwa kuwa bado wapo katika mazungumzo baada ya kumaliza mikataba na klabu hiyo, mambo yamezidi kuwa magumu baada ya pande hizo mbili kushindwa kufikia muafaka.

Awali Yondani alieleza kuwa klabu hiyo inataka kumpa mkataba mpya bila ada ya usajili sambamba na kumtaka kusaini kwa mshahara ule ule aliokuwa akilipwa bila nyongeza yoyote, jambo ambalo hakukubaliana nalo.

Lakini Abdul naye juzi alikutana na hali kama hiyo ya Yondani, jambo ambalo ameweka wazi kuwa hayupo tayari kusaini pasipo ada ya usajili, huku akitaka kuwapo kwa ongezeko la mshahara.

"Nipo tayari kusaini mkataba wa mwaka mmoja, na nimewaambia dau langu ninalotaka ili kusaini, lakini wananiambia nisaini tu mkataba mpya bila ada huku mshahara ukiwa ule ule.

"Nimekataa na ninachosubiri wanilipe hela zangu ninazoidai klabu, wakinilipa basi nitaangalia maisha sehemu nyingine maana nimemaliza mkataba nipo huru," alisema Abdul ambaye msimu uliomalizika, ametoa jumla ya pasi za mwisho sita, akiwa ni beki aliyeongoza kwa pasi za mabao.

Yanga ambayo imesema kwa sasa inageukia usajili wa nyota wa kimataifa, endapo itashindwa na Yondani na Abdul, wataungana na nahodha Papy Tshishimbi kutoka DR Congo ambaye naye amefunguliwa mlango wa kutokea.

Wengine waliachwa ni David Molinga 'Falcao' (DRC) na wazawa Jaffary Mohamed, Tariq Seif, Andrew Vincent 'Dante', Mohamed Banka, Mrisho Ngassa, Ally Mtoni 'Sonso', Muharami Issa 'Marcelo', Ali Ali, Muivory Coast Yikpe Gislain, Mnyarwanda Patrick Sibomana, Mzambia Erick Kabamba na Raphael Daudi.

## AJIBU BADO LULU, AGOMEWA SIMBA

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Simba, Ibrahim Ajibu ataendelea kukitumikia kikosi cha timu hiyo baada ya uongozi wa Namungo FC kugomea ombi la kupewa huduma ya nyota huyo kwa ajili ya kuboresha kikosi chao kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Bara na michuano ya kimataifa, wakati huu ikijiandaa kushiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, alisema walipeleka barua ya kuomba kumsajili Ajibu, lakini Simba imewakatalia ombi lao.

Alisema katika ripoti ya Kocha wao Mkuu, Thierry Hitimana, ilipendekeza majina ya nyota wawili kutoka Simba, Ajibu na Shiza Kichuya, ili kuboresha kikosi chake kuelekea michuano hiyo, jambo ambalo linaonekana kukwama kwa kiungo huyo aliyewahi kuichezea Yanga.

"Katika ripoti hiyo, Hitimana alitaja majina ya wachezaji akiwamo Ajibu na Shiza Kichuya, tumepeleka barua Simba kuomba nyota hao, wametujibu kuwa tutampata Kichuya, lakini si Ajibu kwa kuwa bado yupo kwenye mipango ya benchi lao la ufundi.

"Baada ya kumkosa Ajibu, sasa tunapambana kutafuta mchezaji mwingine, lakini (kocha) amewataka Iddi Mobby wa Polisi Tanzania, Abdulhalim Humud na Issa Rashid ('Baba Ubaya') kutoka Mtibwa Sugar," alisema Zidadu.

Mbali na Ajibu pia alisema wamegonga mwamba katika mpango wa kumsajili Mobby na sasa wanasubiri maombi yao ya kuinasa huduma ya Humud na Baba Ubaya.

"Kuhusu wachezaji wetu, Blaise Bigirima tunatarajia kumalizana naye leo kwa kumwongeza mkataba mwingine baada ya hapo tutaendelea kuwaongezea wachezaji wengine akiwamo Reliants Lusajo pamoja na wale waliopendekezwa katika ripoti ya kocha," alisema mwenyekiti huyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >